SportPesa
TZS. 1,089,062,840
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

**KUTANA NA MANINGO**

Jirani wa mgodini aliyeweka 'ngumu' hesabu ikatimia



BUFE

Ijumaa Aprili 1, 2022 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ulanguzi wa sukari Moshi wamwinua kitini RC kumsaka anayemchezea

**Uungwana wao Unguja wawafanya watalii Ukraine hawataki kuondoka**

Wakataa ofa Ulaya, wahamia Uswahilini

Wenye weledi wa IT waendeleza kazi zao

UKURASA 11

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Ijumaa Aprili 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580902
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kinana, Membe waibua mjadala



Benard Membe



Abdulrahman Kinana

**BARUA** tatu zachochea msamaha CCM, wataalamu wa siasa wakuna vichwa... *Endelea Uk. 2*



Wanataaluma wakitoa heshima zao za mwisho mbele ya majeneza yenye miili ya Prof. Honest Ngowi na aliyekuwa dereva wake, Innocent Mringo, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Watumishi 'hewa' walipwa mamilioni, waziri acharuka

UKURASA 3

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### HUKUMU KESI YA SABAYA MWEZI UJAO

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Mei 31, 2022 inatarajia kutoa hukumu katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa ...

UKURASA WA 5

### WAFUASI WA ZUMARIDI WATAKA KUDHAMINIWA

WAFUASI wa Mchungaji Diana Bundala, maarufu mfalme Zumaridi wameendelea kumkana na kukubali kupata dhamana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, huku wakibadili msimamo waliokuwa nao siku ya kwanza...

UKURASA WA 17

### MWINYI AWAPA SIRI VIONGOZI WA SIASA UTATUZI CHANGAMOTO

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka viongozi wa vyama vya siasa kuzungumzia changamoto zilizopo kwa lengo la kujenga badala ya kushambuliana...



## Serikali: Kifo cha Prof. Ngowi pigo nchini

UKURASA 2

MICHEZO ADEBAYOR TUTALAMBA DUME - SIMBA UK.23 | MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

## Serikali: Kifo cha Prof. Ngowi pigo kwa taifa

Na Waandishi Wetu

SERIKALI imesema taifa limepoteza mtu muhimu katika taaluma ya uchumi kutokana na kifo cha Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Dar es Salaam, Prof. Prosper Ngowi.

Mwakilishi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Jerome Asseyi, alitoa kauli hiyo jana wakati wa hafla ya kuiaga miili ya Prof. Ngowi na dereva wake, Innocent Mringo, iliyofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Asseyi alisema Rais anatoa pole kwa wanafamilia, Chuo Kikuu cha Mzumbe na Watanzania kwa ujumla kwa kumpoteza Prof. Ngowi na dereva wake, akisisitiza kuwa wanatambua mchango wake katika masuala ya uchumi.

"Kwa kweli tumepoteza bingwa wa uchumi, bingwa wa Tanzania. Ni vigumu kuamini kwamba wote hawa wawili hatunao tena, itoshe kusema kwamba tuliwapenda sana lakini Mungu amewapenda zaidi, tuendelee kuwaombea ili roho zao zilazwe mahali pema peponi," alisema Asseyi.

Katika hafla hiyo, Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema kuna haja kuanzisha mradi mkubwa wa kupanua barabara inayotoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ili kupunguza ajali kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa ajali nyingi kwenye barabara hiyo.

"Kwa bahati mbaya takwimu zinaonyesha kwamba hapa Tanzania ajali ndiyo chanzo kikubwa sana cha vifo vya watu wetu, na kwa kweli barabara ya Dar es Salaam, Morogoro mpaka Dodoma ni moja ya njia ambazo zina ajali nyingi na sababu ni kwamba barabara hiyo kwa sasa ina magari mengi.

"Tutumie nafasi hii kama funzo mojawapo, serikali ione haja ya kuanzisha mradi mwingine mkubwa wa kupanua njia hii kwa kiwango cha 'highway' ili kuepusha ajali ambazo zinatokeza," alishauri.

Mbunge huyo alisema Prof. Ngowi alivuka daraja la kuwa mwanataaluma wa kawaida kwa kuwa alikuwa mwalimu darasani lakini na wa jamii kwa ujumla pale alipotoa ujuzi wake wa masuala ya kiuchumi kwa wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, na hata mama ntilie.

"Alitufundisha sisi wanataaluma kuona kwamba haitoshi kuwa profesa tu darasani, tungependa kuona uprofesa wako watu wa kawaida wanafaidika nao kama ambavyo Prof. Ngowi watu walifaidika naye," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Lugano Kusiluka, katika salamu zake kwa waombolezaji, alisema Prof. Ngowi alikuwa mtu mnyenyekevu na mwenye kujishusha kwa kila mtu na alikuwa akimsikiliza mtu wa aina yeyote.

Alisema kuwa Prof. Ngowi alikuwa na mawazo mapya wakati wote na ndiyo maana alikuwa akishirika katika masuala mbalimbali yaliyokuwa na maslahi kwa taifa.

"Prof. Ngowi ni mtu ambaye alikuwa anazungumza na machinga na alikuwa anajua lugha ya kuzungumza nao kama alivyokuwa anazungumza na maprofesa wenzie, wanafunzi wake walikuwa wanafanya mazoezi kwenye ngazi ya chini kabisa, alikuwa ni kiungo kikubwa kati ya chuo na sekta binafsi," alisema. Kiongozi huyo wa chuo alisema watamuenzi na kutumia mawazo yake aliyoyaacha katika maandiko na wataendelea kutumia karama yake ya kujishusha na kuwahudumia watu wa hali ya chini, akiamini kuwa Watanzania wa hali zote kwa ujumla wameshiriki kuwafikisha hapo walipo.

Rais wa Wanafunzi Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndani ya Dar es Salaam, Jonas Baraka, alisema Prof. Ngowi alikuwa anapenda wanafunzi wake na kuwaonyesha mazuri yaliyokuwa yanapatikana katika changamoto.

"Prof. Ngowi alitusisitiza kufanya kazi kwa bidii kwa kuwa ndiyo msingi bora wa maisha, na mara zote alikuwa akituambia tujikite kwenye kutafuta suluhisho na sio kupoteza muda kwenye kuangalia tatizo," alisema huku machozi yakimtiririka.

Akitoa neno la shukrani, mtoto wa Prof. Ngowi, Nana Ngowi, alisema baba yao alipenda kuona wanatimiza ndoto zao, hivyo nao watafanya kila wawezalo kuona malengo ya baba yao juu yao yanatimiza na siku moja waje kuihudumia Serikali ya Tanzania.

Mbali na watendaji na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, hafla ya kuiaga miili hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, asasi za kiraia na viongozi wa dini.

Mwili wa Mringo unatarajiwa kuzikwa leo Moshi mkoani Kilimanjaro wakati mwili wa Prof. Ngowi unatarajiwa kuzikwa kesho kijijini kwao Kibosho wilayani Moshi.

● **Imeandikwa na Jenifer Gilla na Maulid Mbaga**




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza Kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Kinana, Membe waibua mjadala

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi (NEC) imemteua Katibu Mkuu mstaafu wa chama hicho, Abdulrahman Kinana, kuwa mgombea wa kiti cha Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara.

Uteuzi huo unatokana na nafasi hiyo kuwa wazi baada ya Philip Mangula kuandika barua ya kung'atuka na kuiwasilisha kwa Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia Suluhu Hassan.

Mbali na hilo, NEC imewasamehe na kuwarudishia unachama wao Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe, na aliyewahi kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, Abdallah Maulid Diwani, baada ya kuandika barua mara tatu kuomba kusamehewa.

Hata hivyo, uamuzi huo umekosolewa na baadhi ya wachambuzi wa siasa nchini, wakinyoshea kidole viongozi waandamizi wa CCM kuendelea kupewa nafasi za uongozi wa juu kwamba kunaminya nafasi za uongozi kwa kizazi kipya.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema NEC imepokea barua rasmi ya kung'atuka kwa Mangula aliyomwandikia Rais Samia na kuiwasilisha mbele ya kikao cha NEC kwa ajili ya kukidhi matakwa ya kikatiba na kanuni.

"Mangula amefikia uamuzi huo ili kukidhi matakwa ya kikatiba ibara ya 19(e) ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977 pamoja na kanuni ya 116(b) ya Kanuni za Uchaguzi za CCM toleo la mwaka 2017, baada ya kupokewa kwa barua na kuridhiwa nafasi ya Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara imetangazwa kuwa wazi.

"Ibara za 105 na 106 za kanuni za uchaguzi, pia Katiba ya CCM ibara ya 100(5)(a), ibara ya 114(1) ya Katiba ya CCM mwaka 1977 toleo la mwaka 2020, Makamu Mwenyekiti atachaguliwa na mkutano mkuu taifa," Shaka alisema.

Aliongeza kuwa katika kukidhi matakwa hayo ya kikatiba, wajumbe wa NEC baada ya kupokea ombi hilo la kung'atuka kwa Mangula, wamefanya uteuzi wa mwanachama wa CCM ambaye atapelekwa kwenye mkutano mkuu kwa ajili ya kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara.

"Hayo yamefanyika ili kukidhi matakwa ya katiba, Halmashauri Kuu ndio yenye jukumu la mwisho la kuteua jina moja la mgombea wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara.

"Ninayo furaha kuwajulisha kwamba NEC imepitisha na kumteua Kinana ambaye ni Katibu Mkuu mstaafu wa CCM, kuwa mgombea wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara na uchaguzi wake utafanyika kesho (leo) kupitia mkutano mkuu maalumu wa CCM," alisema.

Shaka alisema Rais amemshukuru Mangula kwa utumishi wake uliotukuka, akitumikia nafasi hiyo kwa miaka 10 tangu mwaka 2012 na ameng'atuka kwa hiari yake.

"Wakati Mangula anang'atuka leo (jana) ametimiza miaka 81 kwa kuwa ni siku yake ya kuzaliwa, ametumia muda wake kukijenga na kuimarisha CCM," alisema.

### MEMBE ASAMEHEWA

"Mtakumbuka ndugu Benard Membe alikuwa mwanachama wa CCM na baada ya yale yaliyotokea, ndugu Membe aliondoshwa au kufutiwa uanachama wake ndani ya CCM, pia yupo ndugu mwingine anaitwa Abdallah Maulid Diwani, aliwahi kuwa Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe, naye mwaka 2018 alifutiwa ama kuondolewa uanachama wake wa CCM."

"Kuanzia leo (jana), ndugu Benard Membe na Abdallah Maulid Diwani ni wanachama wa CCM na taratibu nyingine za kupatiwa kadi za uanachama zitafanyika kwenye maeneo yao kama ambavyo Katiba yetu imeelekeza," alisema.

### BARUA TATU

Alisema wanachama hao waliandika barua za kuomba kusamehewa zaidi ya mara tatu ndani ya CCM na kwa nyakati tofauti walikuwa wakiomba kuonana na viongozi wa chama ili kuelezea hisia zao na kuelezea utayari wao wa kurudi kuungana na wanachama wenzao.

### WACHAMBUZI WA SIASA

Mchambuzi wa siasa, Gwandumi Mwakatobe, katika mazungumzo na Nipashe kuhusu uamuzi huo wa CCM, alisema kinachoonekana vyeo vyote isipokuwa cha Mwenyekiti ndani ya CCM vinazunguka kwa watu wale wale na wachache sana na wa kizazi kipya wanaofanikiwa kupenya.

Alirejea kuwa Mangula alishika nafasi ya Katibu Mkuu wa CCM kwa muda mrefu na vyeo vingine, hivyo haishangazi kuona Kinana anapewa cheo kinachoachwa na Mangula.

"Hii inaonyesha suala la kukuza na kuendeleza vizazi linapokuja kwenye nafasi za juu litachukua muda mrefu, ikiwa CCM hata vyama vya upinzani kwamba mwenyekiti anakuwa yule yule, viongozi wazuri huweza kutengeneza viongozi wazuri ikiwa watataka kufanya hivyo, lakini tunadhani wataendelea kuwa hao hao, sifa mojawapo ya kiongozi bora ni kuzalisha viongozi wengine wazuri," alisema.

Mtaalamu huyo wa sayansi ya siasa alisema Kinana alifanya kazi nzuri na alishika nafasi nyingi kuanzia jeshini lakini kuendelea kuwa na watu wale wale kunaziba nafasi za ukuaji wa chama kwa kukaribisha mawazo mapya.

"Vizazi vinapaswa kubadilishana kupata mawazo mapya, ni ngumu sana kuwa na mawazo mapya na watu wale wale, mawazo mengi ya ukiritimba yanatokea ikiwa watu ni wale wale, hawazai watu wapya, suala siyo kubadilisha watu, bali kubadili mitazamo inayoendana na wakati mpya na vizazi vipya," alifafanua.

Mwakatobe alisema kila kizazi kiibuke na watu wapya wanaoweza kujifunza na waliotangulia na wanao wajibu wa kuzalisha viongozi wapya.

"Hata ukiwa na mifumo mipya, ukibadili katiba na watu ni wale wale, ni sawa na kumbadilishia mchungaji au shekhe kanzu ila akawa ni mtu yule yule," alihitimisha.

### UVCCM WAPANGUANA

Katika hatua nyingine, jumuiya mbili za chama hicho ambazo ni Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) na Jumuiya ya Wazazi zimefanya mabadiliko ya nafasi mbalimbali ikiwamo makatibu wa jumuiya hizo.

Kwenye taarifa iliyotolewa na Katibu wa UVCCM, Khenani Kihongosi, ilionyesha kuwa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa iliyoketi juzi ilifanya uteuzi wa baadhi ya Makatibu wa UVCCM Wilaya na wengine kuwabadilishia vituo vya kazi.

Jumuiya ya Wazazi katika taarifa iliyotolewa na Naibu Katibu Mkuu Bara, Daniel George, pia ilisema sekretarieti hiyo imeteua makatibu wa jumuiya hiyo wilaya na baadhi ya watumishi wanakwenda makao makuu ya jumuiya.

Mkutano huo pamoja na kufanya uchaguzi wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, pia utawapokea wanachama hao waliosamehewa na kufanya mabadiliko ya Katiba ya CCM.

# Watumishi 'hewa' walipwa mamilioni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini Mamlaka za Serikali za Mitaa 25 zilifanya malipo ya Sh. milioni 556.84 kwa watumishi waliostaafu kufariki, kutoroka, kuacha kazi na waliokuwa likizo bila malipo.

CAG Kichere alieleza hayo juzi alipokuwa akiwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino.

Pia alisema Mamlaka 24 za Serikali za Mitaa zilitumia Sh. milioni 664 katika matumizi yasiyo na manufaa kama malipo kwa bidhaa ambazo hazijawahi kupokelewa, riba na adhabu, kuchelewesha malipo na malipo ya posho kwa watumishi wasiostahili.

Kuhusu ukusanyaji wa mapato, alisema makusanyo kwenye mamlaka za serikali za mitaa 147 hawakuwasilisha benki makusanyo ya Sh. bilioni 17.

Kadhalika, alibaini uwapo wa tozo za riba kutokana na kuchelewesha malipo kwa makandarasi katika miradi mitano inayotekelezwa chini ya sekta ya usafirishaji na kusababisha tozo ya riba ya Sh. bilioni 4.79.

"Wakala wa Barabara TANROADS na TARURA (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini) walitozwa riba ya Sh. bilioni 69.62 kwa kuchelewesha malipo ya madeni Sh. bilioni 673.52 makandarasi na washauri wa ujenzi kati ya kiasi hicho deni la Tanroads ni Sh. bilioni 664.35 iliyosababisha tozo ya riba ya Sh. bilioni 68.7 zilisababisha na utoaji wa fedha zisizoridhisha serikalini," alisema.

Alieleza kuwa mashirika matatu ya umma yalichelewesha malipo kwa zabuni baada ya kupata bidhaa au huduma mbalimbali hivyo kutozwa riba na adhabu za Sh. bilioni 95.2 ambapo hakuna thamani ya fedha iliyopatikana kwenye gharama hizo.

Kuhusu ukaguzi wa Ofisi za Balozi, CAG alisema balozi 10 zina viwanja ambavyo havijaendelezwa pamoja na kutolea taarifa kwenye ripoti zake hadi sasa hakuna hatua zilizochukuliwa.

Alisema Balozi 10 zimekodi nyumba za ofisi na kugharamia Sh. bilioni 3.6 kama kodi kwa mwaka 2020/21 na kwamba fedha zingeokolewa kama balozi zingejenga majengo yao.



Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (Uchumi na Huduma za Kifedha), Dk. Yamungu Kayandabila (kushoto), Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda cha Sukari cha Kagera Sugar Ltd (KSL), Seif Ali Seif (wapili kushoto), Naibu Gavana Mkuu (Utawala na Udhibiti wa Ndani) Julian Banzi Raphael (watatu kushoto) na Naibu Gavana (Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha), Dk. Bernard Kibese (wanne kushoto), wakimsikiliza Mtaalamu wa Kilimo Mwandamizi wa KSL, Erica Mwakisinini, wakati wakurugenzi wa bodi wa benki hiyo, walipotembelea kiwanda hicho, mkoani Kagera juzi.
**PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# CAG abaini mabilioni hayajawasilishwa BoT

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere, amebaini akaunti za makusanyo za taasisi za umma 68 hazikuwahi kuhamisha fedha kwenda Benki Kuu (BoT) tangu zianze kukusanya mapato.

Pia amebaini uwapo wa mifumo ya kielektroniki inayofanya kazi zinazofanana ikiwamo mifumo ya kihasibu.

CAG Kichere alibainisha hayo juzi alipowasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, Ikulu Chamwino.

Alisema hadi kufikia Mei, 2021, akaunti hizo zilikusanya Sh. bilioni 148.81, Dola za Marekani milioni 6.33 na Euro milioni sita.

"Imetokana na maofisa masuhuli wa taasisi husika kutoweka agizo kwa benki za biashara kuhamisha makusanyo kwa benki za biashara kwenda benki kuu kama ilivyo kwenye maelekezo," alisema.

Pia alibainisha upungufu kwenye mfumo wa malipo ya serikali (GePG) ambapo serikali haijakamilisha uhakiki wa mapato kupitia benki za biashara kama yamehamishwa yote kupelekwa Benki Kuu, hali inayochelewesha serikali kupata fedha kwa wakati.

"Mfumo unaruhusu benki ya biashara kusitisha akaunti za makusanyo kabla ya kuhamisha bakaa kwenye akaunti hizo kwenda Benki Kuu, kuruhusu usitishwaji wa akaunti ambayo ina bakaa kunaweza kusababisha fedha hizo kutumika vibaya," alisema.

CAG Kichere alisema miamala 225 yenye thamani ya Sh. milioni 115.2 kwenye mfumo wa mapato wa LGRSIS unaotumiwa na halmashauri ilikuwa na namba za malipo zilizoisha muda wake za mfumo wa GePG.

Kuhusu mifumo, CAG alisema kuna mifumo ya uhasibu zaidi ya mmoja inayotumiwa na taasisi za serikali na Wizara ya Fedha imeidhinisha matumizi ya mifumo mitatu.

Alisema uwapo wa mifumo mingi unatoa mianya ya upotevu wa mapato na kwamba mifumo yenye kazi moja ni matumizi mabaya ya rasilimali.

# Bashungwa awapasha watumishi wazembe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amesema mtumishi wa umma atakayebainika kukosa uadilifu ataondolewa kazini.

Bashungwa aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kupokea ripoti ya ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21.

Alisema kwa wale wachache ambao watashindwa kuwa waadilifu na kwenda na mwelekeo wa Rais katika kutoa huduma kwa wananchi, atawachukulia hatua.

"Jambo hili sio kushusha vyeo tu, bali kuwaondoa kwenye utumishi wa umma kwa wale watumishi ambao hawatakuwa hawatoshi kwa namna yoyote, ile tabia ya kushusha vyeo na kuwahamisha ndani ya serikali hilo halitavumilika chini ya usimamizi wangu wa hii wizara, kwa wale ambao watakuwa hawatoshi ni kuwatoa kwenye utumishi wa umma," alisema.

"Tunashirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi kuhakikisha tunaomba vibali vya ajira, wako Watanzania wengi, wasomi na wazalendo ambao wako mtaani wanatafuta kazi na wako tayari kuwatumika Watanzania kwa uaminifu mkubwa. Hivyo ni matarajio yangu tutabadilika."

Aidha, Bashungwa alisema baada ya kukamilisha kazi ya kushughulikia maofisa manunuzi kwenye halmashauri sasa anakwenda kwa waweka Hazina na kuagiza taarifa kamili ya kazi hiyo ifike ndani ya siku tatu mezani kwake.

"Tumejipanga vyema kuhakikisha tunatekeleza maagizo ya Mheshimwa Rais na dhamira yake ya kuhakikisha Ofisi ya Rais-TAMISEMI inawahudumia Watanzania vilivyo, na katika hili nimhakikishie mheshimwa Rais kwamba maagizo yake ambayo ameyatoa kuhusu weledi na uadilifu wa watumishi wa umma wakati anapokea ripoti ya CAG na TAKUKURU, mimi nitaanzia hapa ninapopasimamia," alisema.

KUTANA NA SADOCK MANINGO

# Jirani wa mgodini Mara aliyewawekea ‘ngumu’ wawekezaji na hesabu ikatimia

## ● Ajiandaa kuhama kwa staili ‘sina haraka’

**Na Mwandishi Wetu,** TARIME

SAKATA la mvutano kati ya wamiliki wa mgodi wa dhahabu North Mara na wenyeji waliowakuta na kuwakaribisha jirani nao, lina sura pana.

Kati ya hao, wapo waliokuwa wepesi kunyosha mikono kwa wageni hao, lakini kuna Sadock Maningo, baba wa watoto sita, nusu yao ni mabinti, naye umri wake sasa unasajili mwaka wa 49, msimamo wake ni mkali kwa kilicho chake.

Hapo ni penye Kitongoji cha Kigonga B kilichoko katika Kijiji cha Matongo, Kata ya Matongo wilayani Tarime, umbali wa Km 85 kusini mashariki mwa Mji wa Tarime.

Kwa kurejea anakoishi, huyo ni jirani hasa kwa maana ya jirani na mgodi wa Barrick North Mara, yeye akiwa kwenye upande mmoja wa mwinuko, huku kipande cha mgodi ambako udongo unaochimbuliwa unamwagwa, ndiyo ujirani wao unakoanzia ukiwa upande wa pili wa mwinuko.

Ukiondoa bonde dogo linalotenganisha pande hizo mbili za majirani, kwa tathmini ya kisomi ambayo ushuhuda wa Nipashe uliufanyia kazi, kwa umbali wa tambarare kunahitajika hatua 300 za mtu mzima kufikia ng’ambo ya pili.

Makazi anakoishi Maningo yanaundwa na nyumba tatu zilizokamilika na moja ujenzi haujaisha, umepigwa ‘stop’ na yanayojiri katika msuguano wa ujirani huo.

Jengo moja lina ramani ya ‘L’ ndilo analoishi na lingine lenye ramani ya asili ya Tarime - nyumba ya duara, mwenyewe anasema ni mahususi kwa wageni na iliyopigwa ‘stop’ ndiyo nyumba kubwa aliyonuia ingekamilika angehamia, usafiri wake mkuu ni pikipiki binafsi jamii ya bodaboda.

Majengo hayo ambayo yote ni ya matofauli ya kuchoma na kuezekwa kwa bati, ipo nyumba ya nne iliyoko katika mtindo wa ‘mgongo wa tembo’ ikiwa na ukubwa wa wastani na ina vyumba vitatu.

**SURA YA MSUGUANO**

Kuna methali isiyo rasmi kwamba nyumba ni mtu na mtu ni nyumba zaidi, kwa maana hiyo makazi hayo ni Maningo, ambaye siyo siri ni ‘shoka’ na wa kipekee kijijini Matongo.

Naam! Upekee wake una sifa moja tofauti na wenzake. Amekuwa mgumu kuhama ‘kienyeji’ kwani yeye kwa haki yake ‘piga ua’ haitoki kwa makubaliano mepesi na kuujua ukweli huo, mpaka sasa makazi yake pekee ndiyo yamebaki majirani wa mgodi huo maarufu.

Kisa na mkasa? Mwenyewe anaweka wazi kwamba hakuwa tayari kwa fidia zisizoeleweka, jambo ambalo lilimwingiza kwenye mvutano wa muda mrefu na walipaji fidia hao.

Maningo mwenye wajihi wa kuvaa ama koti refu kwa siku za kawaida na zile rasmi, ikiwamo kwenda kuabudu, anaonekana ndani ya mashati ya vitenge, daima ana sifa kuu ya kwanza kuzungumza kwa kujiamini mno.

Pia wakati wote anapotoa ufafanuzi, anakuwa kwa sauti ya juu, akitumia marejeo mbalimbali ambayo mara zote hayuko mbali nayo na kisha kuijaza sentensi yake itimie kwa kauli za viongozi wa kitaifa.

Lingine analosisitiza kwa uchungu, akiweka marejeo ya historia mbalimbali ya kwenda kulalamika kwenye ofisi za Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Tarime, hata kufunga safari hadi Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, anaisimulia Nipashe kuna mambo yanayomwacha katika mantiki ya kiulizo, hasa kwenye anachokipazia sauti “...ardhi yangu ilivyopimwa siridhiki...”

Ni kupitia msimamo huo, ndipo anasema hata wawekezaji wa Barrick North Mara walipokuja na hoja sasa ‘achukue chake’ ahame mahali hapo, akawa mgumu.

Anakiri haina maana kwamba mambo yaliendelea kuwa mepesi kwake, hasa pale wakazi wenzake walipopiga saluti kwa ‘kuchukua chao’, yeye akibaki anasema ameteseka kimazingira kutoka kelele za mgodini, mitetemo hata athari za mionzi lakini ‘akikomaa tu’.

Hatua ya kwanza ya mwafaka wake na mgodi alipoelezwa tathmini ya makazi yake ilikuwa jumla ya Sh. milioni 129.9354 mnamo Septemba 2019, naye akaridhia, alishangaa sana siku ya kwenda kutia saini akakutana na tarakimu mpya, Sh. milioni 62.905, ikiwa ni pengo la wastani Sh. milioni 67.

Hapo hapo akiwa kwenye ofisi za wawekezaji migodi hapo, akabadilika na kuwa Maningo ‘orijino’ kwani alikataa katakata kusogeza mkono wake kwenye peni kuhalalisha pengo la Sh. milioni 67 kutoka kwenye miliki yake.

Ni hatua iliyozua mgogoro mpya iliyoendana na vikao vingi vya mwafaka nenda rudi, hata kukafanyika tathmini nyingine hatimaye mnamo Mei mwaka jana, ikiwa ni mwaka mmoja na miezi minane imevuka, maelewano yakafikiwa tathmini ya makazi mara hii ikitamkwa ni Sh. milioni 83.7.

Hapo tena Maningo akacharuka kwa msimamo wake uleule, ilhali wakati huo wenzake walishabeba vyao, wako katika maisha mapya kwingineko, yeye akiendeleza msimamo imekuwaje safari hii makazi yamechuja thamani kwa kiwango cha Sh. milioni 46 na ushee? Akatamka “haiwezekani”.

Baada ya hatua hiyo, miezi saba baadaye Maningo alidumu na msimamo wake akihitaji Sh. milioni 129, huku walipaji wakisimama kwenye alama yao ya Sh. milioni 83.7: Ni vuta nikuvute baina ya mwenyeji na mgeni, mkazi na mwekezaji.

Muda wote mkazi huyo akiendelea kupambana na usumbufu wa kelele, mitikisiko ya ardhi, kuishi peke yake bila jirani, akidumu katika msimamo wake “heri kufa nikitetea changu’, akaanza kupata magumu ndani ya familia, mwenza wake akiugua.

Maningo anasema hapo ndipo mke huyo akaanza kumshawishi apokee walau pesa hizo ambazo hajaridhika nazo, lakini itakuwa na maana kwao hasa katika kumtibu mama huyo mgonjwa.

Kwa mujibu wa Maningo, huo ndiyo ukawa mwanzo wake wa kulegeza msimamo na hata baada ya majadiliano ya kina ndani ya nyumba, alifunga safari hadi mgodini Barrick North Mara na kueleza azma, hata akapokea peni kutia saini kuridhia malipo ya Sh. milioni 83.7.

Hiyo ilikuwa Desemba 30, mwaka jana kwa maana ya kwamba ameupokea mwaka mpya akiwa tayari ana kitita chake kwenye akaunti.

Kwa mujibu wa Maningo, wepesi wa malipo hayo uliwezekana kupitia shinikizo la kisheria kuhamia mahakamani, lililotolewa na wadhamini wake, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ukweli ambao taasisi hiyo imeithibitishia Nipashe.

**MSIMAMO WA LHRC**

Joyce Komanya, Ofisa Mipango Mwandamizi wa LHRC anayeshughulika na haki, uwajibikaji na mazingira, katika taarifa yake rasmi kuhusu sakata hilo, anatamka:

“Haki ya kumiliki mali ikiwamo ardhi ni haki ambayo imeainishwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Migogoro ya ardhi imeendelea kushamiri baina ya wawekezaji na wananchi kwenye maeneo ya Kanda ya Ziwa.

“Kutokana na taarifa na changamoto hizo, LHRC kwa mamlaka iliyonayo, inapigania haki za watu ambazo zimepokwa kutokana na shughuli za uwekezaji kwenye maeneo yao.

“Maeneo hasa ya migodini yameripotiwa kuwa na changamoto nyingi za ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwamo haki ya kumiliki mali.

“Hivyo basi, LHRC inatoa rai kwa serikali kuweka vipaumbele kwa wawekezaji kuheshimu misingi ya haki za binadamu kwa kuhakikisha utu wa mtu unalindwa na kuzingatiwa.

“Kushindwa kutoa fidia stahiki na kwa wakati sahihi kwa wamiliki wa ardhi kwenye maeneo ya uwekezaji ni kupoka haki ya kumiliki mali kwa watu wao na kuwafanya washindwe kuishi maisha yenye staha kwa ustawi wao na wa watoto wao.”

**MAISHA MAPYA**

Je, anafanyia nini? Maningo ameidokeza Nipashe kwamba hadi sasa anaendelea na ujenzi kwingineko ambako si mbali sana, hata hivyo hadi sasa bado ni mkazi wa makazi yaleyale.

Pia, kama alivyo mzazi yeyote, Mzee Maningo anadokeza kuwa ana watoto kadhaa wanaosoma kwenye shule iliyo jirani na makazi yake, ambayo nayo iko katika ajenda ya kuhamishwa, jambo ambalo analitaja limo katika orodha ya yanayomuuza kichwa, ndani ya mustakabali wa sakata hilo.



Sadock Maningo, akiwa kwenye himaya ya makazi yake anakotakiwa kuhama. Picha ndogo akionyesha nyaraka za malipo **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Vituo maalumu 15 vya bodaboda kujengwa Dar es Salaam

**Na Romana Mallya**

HALMAUSHARI ya Jiji la Dar es Salaam ipo katika mchakato wa kutenga vituo maalumu 15 kwa ajili ya waendesha pikipiki za biashara, maarufu bodaboda, ambao watahudumia wateja wanaotoka katikati ya jiji.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri, alisema vituo hivyo vitatengwa kwenye barabara zinazoingia katikati ya jiji hilo la kibiashara.

"Lengo ni kuwe na vituo kama 15 ambavyo, tumekubaliana viwe kwenye barabara zinazoelekea katikati ya jiji, ni maeneo gani, bado hatujakubaliana na watu wa bodaboda wenyewe. Bodaboda walikuwa wanataka waingia mpaka katikati ya jiji na tulisema wasiingie katikati.

"Vituo bado hatujakubaliana, vikikamilika tutawaambia, tunapanga mji kwa ushirikiano na wenye bodaboda, hivyo vitakuwapo vituo 15 ambavyo tumeviainisha, maeneo gani vitakuwa tunaendelea kuzungumza nao," alifafanua.

Alisema walifikiria kwamba wenye bodaboda wasiingie katikati ya mji, wawe wanashusha abiria maeneo maalumu yatakayotengwa.

"Tulifikiria mfano maeneo ya Kamata au kama unaingia mjini kwa kutokea Magomeni bodaboda wanabaki eneo la Fire, hapo ndipo anachukua watu kutoka katikati ya jiji kuwapeleka nje ya jiji.

Alisisitiza kuwa suala hilo bado hawajakubaliana na wenye bodaboda na watakapofikia mwafaka, wataelekeza.

Shauri alisema kwa sasa watu wake kwa kushirikiana na wenye bodaboda wanamalizia mchakato huo.



Abiria akiingi kwenye daladala kwa kupita dirishani katika kituo cha Mbezi Mwisho kuelekea Gongo la Mboto kupitia Barabara la Malamba Mawili, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wafuasi wa Zumaridi waendelea kumkana, wakubali kudhaminiwa

**Na Richard Makore,** MWANZA

WAFUASI wa Mchungaji Diana Bundala, maarufu mfalme Zumaridi wameendelea kumkana na kukubali kupata dhamana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza, huku wakibadili msimamo waliokuwa nao siku ya kwanza wa kutokuwa tayari kudhaminiwa na kumuacha Mungu wao.

Kwa mara ya kwanza Machi 3, mwaka huu, wafuasi 92 pamoja na Zumaridi walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza na kusomewa mashtaka matatu.

Mashtaka hayo ni pamoja na kushambulia polisi, kuzuia polisi kufanya kazi yao na kusafirisha binadamu ambalo linamkabili Zumaridi peke yake.

Siku ya kwanza mfuasi mmoja alikubali kudhaminiwa na kubaki 91 waliokataa dhamana licha ya kuwa ilikuwa wazi.

Wafuasi hao walidai wapo tayari kwenda Gereza la Butimba, mkoani Mwanza pamoja na Zumaridi na kwamba hawatakubali kupewa dhamana na kumuacha peke yake.

Baaada ya hapo wafuasi wengine walibadili msimamo wao wa awali na kuendelea kudhaminiwa na jana wanane walikubali na kupata dhamana na kufanya idadi ya waliobaki gerezani na Zumaridi kuwa sita.

Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani Machi 3, mwaka huu, ikiwa ni siku saba tangu walipokamatwa nyumbani kwa mchungaji huyo eneo la Buhongwa, jijini Mwanza.

Mchungaji huyo ambaye ana wafuasi wengi katika kanisa lake, jana alionekana mahakamani hapo akiwa amejifunika 'gubigubi' kwa kitenge, huku Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mwanza, Stella Kiama, akiwaonya waandishi wa habari kumpiga picha mshtakiwa huyo akiwa kizimbani.

Aliwaambia waandishi wa habari wasithubutu kupiga picha mshtakiwa akiwa kizimbani kwa kuwa yatakayowakuta itakuwa ni hasara kwao.

Hatua hiyo ilifuatia wakili wa washtakiwa hao, Eric Muta, kulalamikia kwamba mshtakiwa namba moja, Zumaridi alipigwa picha akiwa kizimbani na picha zake zikaonekana kusambaa katika mitandao ya kijamii, Machi 17, mwaka huu.

Licha ya wafuasi hao kuendelea kumkana Zumaridi ambaye wanamuita mungu wao chini ya jua, washtakiwa hao walishindwa kusomewa maelezo ya awali kutokana na wenzao watatu kutofika mahakamani pamoja na hakimu wao kupata udhuru.

Wakili wa serikali mwandamizi, Emanuel Luvinga, aliiambia mahakama hiyo kwamba kutokana na hali hiyo, ipangwe siku nyingine ili washtakiwa waweze kusomewa maelezo ya awali huku akisema mshtakiwa namba moja upelelezi wa kesi yake haujakamilika.

Wakili Luvinga aliwaonya wafuasi hao kuacha visingizio vya aina yoyote labda iwe ugonjwa cha kumzuia mshtakiwa kufika mahakamani.

Katika kesi hiyo, Zumaridi alinyimwa dhamana kwa kuwa kosa la usafirishaji binadamu halina dhamana kwa mujibu wa sheria.

Siku ya kwanza washtakiwa wote baada ya kuulizwa na hakimu kama walitenda makosa hayo, walikana.

Wakili Luvinga aliiambia mahakama hiyo kwamba, kesi namba 10 ya mwaka 2022, inamhusu mchungaji Diana Bundala na wenzake wanane ambao wanadaiwa kufanya shambulio la kuzuru mwili na kuzuia maofisa wa polisi kufanya kazi.

Alisema kesi namba 11 ya mwaka 2022, inamhusu Mfalme Zumaridi peke yake ambayo ni usafirishaji haramu wa binadamu na kesi namba 12 ya mwaka 2022 inamhusu na wenzake 84 wanaodaiwa kufanya kusanyiko lisilo halali.

Mwishoni mwa mwezi wa Februari, mwaka huu, washtakiwa hao walikamatwa nyumbani kwa mchungaji huyo na Jeshi la Polisi, mkoani Mwanza na kushikiliwa kwa siku saba kabla ya kufikishwa mahakamani.

Kesi hiyo imepangwa tena kuendelea katika mahakama hiyo, Aprili 14, mwaka huu kwa washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

# Hukumu ya kesi ya Ole Sabaya itakuwa mwezi ujao

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Mei 31, 2022 inatarajia kutoa hukumu katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita.

Ole Sabaya na wenzake, katika kesi hiyo, anakabiliwa na mashtaka matano yakiwamo ya utakatishaji wa fedha, matumizi mabaya ya madaraka, kuunda genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Washtakiwa wengine ni Lengai Ole Sabaya, Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), John Odemba, Watson Mwahomange na Nathan Msuya (31).

Hakimu wa mahakama hiyo, Dk. Patricia Kisinda, alisema jana kuwa hukumu ya kesi hiyo, inatarajiwa kutolewa Mei 31, mwaka huu.

Katika hatua nyingi, mshtakiwa wa tatu katika shauri hilo, Watson Mwahomange, alishindwa kufika mahakamani kwa madai ni mgonjwa. Ofisa wa Magereza, Inspekta Ramadhani Misanga, alidai kwamba walimwacha mahabusu mshtakiwa huyo kwa kuwa alikuwa anaumwa. "Niliitwa na Mganga Mkuu wa Magereza, alinieleza kuwa Watson anaumwa na alinipatia cheti cha kuthibitisha kwamba ni mgonjwa," alidai Misanga.

Kadhalika alidai kwamba walipewa submission za mshtakiwa huyo (Majumuisho ya Mwisho), lakini hayajasainiwa hivyo aliiomba mahakama kuwaruhusu kwenda kumsahinisha ili yawasilishwe mahakamani.

Baada ya ombi la ofisa huyo wa Magereza kuomba kupewa muda wa kwenda kumsahinisha mshtakiwa huyo, Hakimu Kisanda, alitoa muda wa siku moja kwa Watson kuhakikisha anawasilisha majumuisho ya mwanzo.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, na ni kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B,2) sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019. Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linamkabili Sabaya peke yake, kinyume na kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linawakabili washtakiwa wote saba, ni kinyume na kifungu 12(D), 13(1A), cha Sheria ya Utakatishaji Fedha sura ya 423 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunahitaji kuwawajibisha waliotajwa ripoti ya CAG

**UKISOMA** ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mwaka 2020/21, kila eneo alilokagua amekuta upigaji mkubwa, ikimaanisha fedha inayoingia serikalini inatoka kwa mlango mwingine ambao unakwenda kunufaisha baadhi ya watu, huku wanaotakiwa kunufaika hawanufaiki.

Mawanda ya ukaguzi wa CAG hujikita kwenye serikali kuu, serikali za mitaa, taasisi na mashirika ya umma na vyama vya siasa, yaani kokote fedha ya umma ilikokwenda lengo ni kuwa na uwajibikaji na kuhakikisha kila shilingi inatumika vizuri.

Kila mwaka CAG huweka hadharani ili serikali ijue hali halisi na ichukue hatua, mara zote imekuwa kawaida kuonekana mchwa wanaendelea kujiimarisha badala ya kupungua au kwisha, licha ya kusomesha wataalamu, kuwa na sheria, kanuni na sera za kuongoza matumizi ya fedha ya umma.

Mathalani, kati ya taasisi 19 za umma 999 zilizokaguliwa mwaka 2020/21 zilizopata hati zenye mashaka ni sita na ambazo CAG alishindwa kutoa maoni ni nne. Alimweleza Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa walikagua mifuko ya hifadhi ya jamii ya NSSF na PSSSF wakabaini mafao ya pensheni yanazidi mapato yatokanayo na michango ya wanachama.

Vyama vya siasa vilivyokaguliwa vilivyopata hati yenye mashaka ni CUF, UDP, SAU huku hati mbaya ni ADC, CHAUMMA, UMD, TLP na Chama Cha Demokrasia Makini huku akishindwa kutoa maoni kwenye hesabu za AFP.

Kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, walibaini Sh. bilioni 47.07 zilizokopeshwa kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu hazikurejeshwa.

Hili ni jambo la kusikitisha kwa kuwa fedha hizi zilipaswa kurejeshwa ili wakopeshwe wengine na kuona thamani ya fedha kwa kuangalia mabadiliko kwa waliokopeshwa, lakini kwa kutorejeshwa inaonyesha kuna tatizo mahali lazima lishughulikiwe. Mathalani, wakati wa mkutano wa sita wa Bunge, baadhi ya wabunge walisema mikopo hiyo inashindikana kurejeshwa kwa kuwa waliokopeshwa sio wanufaika bali kuna watu wameunda vikundi na kuzichukua huku wakitakiwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza.

Fedha hizo zinatukumbusha mabilioni ya JK (Jakaya Kikwete) ambayo yalitolewa kwa kila mkoa kukopesha makundi maalum ziliishia kupigwa kiasi cha lengo kitofikiwa. CAG alisema halmashauri 83 hazikuchangia Sh. bilioni 6.68 ya asilimia 10 ya bajeti yao kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kusaidia makundi hayo kubadilisha maisha yao.

Pia alibaini halmashauri zilifanya malipo ya Sh. milioni 556.84 kwa wastaafu waliofariki, kutoroka, kuacha kazi na waliokuwa likizo.

Alibaini matumizi yasiyo na manufaa yaliyofanyika kwa bidhaa ambazo hazijawahi kutolewa, huku kukiwa na matumizi ya fedha mbichi (fedha ambazo hazijapelekwa benki) zaidi ya Sh. bilioni 17 kwa halmashauri 147.

Kwa ujumla huu ni upigaji ambao kimsingi unakatisha tamaa walipa kodi wa nchi hii, ambao wanataka kuona fedha wanayotoa inasimamiwa vyema, inafanya kazi inayotakiwa na sio watu wachache kuiba wazi wazi na kunufaika wakati wengi wanaumia.

Fedha zilizoibwa zingeweza kununua vifaa tiba, dawa na kujenga majengo ya zahanati, vituo vya afya na hospitali, pia vingeongeza miundombinu ya shule na barabara, ili Watanzania wote wanufaike na keki ya taifa, lakini zinapigwa na wachache kwa manufaa ya wachache.


Ni muhimu walipa kodi wakaona uwajibikaji wa wazi wa kila shilingi yao, kwamba watu wakamatwe na kufikishwa mahakamani, lakini mali walizopata kwa njia haramu zifilisiwe kwa kuwa wametudhulumu Watanzania licha ya imani tuliyokuwa nayo kwao.

Bila hatua madhubuti kuziba mianya ya upotevu wa mapato hali itaendelea kuwa hii ambayo itakatisha tamaa, itaonekana serikali ni shamba la bibi kwamba mtu anaweza kuingia kwa ujanja wake akachota fedha akazitumia na kuendelea na maisha kama kawaida.

Tunaona umuhimu wa kuwawajibisha wote wanaotajwa katika ripoti ya CAG kwa kuwa ofisi hiyo ni chombo kilichopewa mamlaka hiyo, na kinatekeleza majukumu yake kwa weledi na utaalamu wa hali ya juu. Kwa lugha rahisi hakuna sababu ya kuwataja waliohusika kufanya ubadhirifu wa fedha za walipa kodi halafu hatua za kuwashughulikia zikachelewa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Sasa Rais kafafanua inatosha sana, kilichobaki tufanye kazi zetu

Na Adam Fungamwango

**SASA** nadhani kila mmoja anatakiwa arudi na kufanya kazi yake kwa bidii, badala ya kuendelea kulalamika juu ya kupanda kwa mafuta na baadhi ya vitu nchini.

Wakati wa kukabidhiwa ripoti ya Mdibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), Charles Kichere, Ikulu Chamwino Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan amefafanua vizuri ni kwa nini bei za vitu mbalimbali zimeanza kupanda nchini.

"Sasa hivi ukisoma maoni mengi ya Watanzania kuna malalamiko ya kupanda kwa bei za bidhaa. Lakini wote tunajua baada ya COVID-19, dunia yote imekuwa na mfumuko wa bei, kwa sababu bidhaa zote zilizokuwepo maghalani, zilitumika ndani ya miaka hii miwili mitatu ambayo dunia ilikumbwa na COVID," alisema Rais.

Kwanza kila mtu anafahamu juu ya janga la ugonjwa wa UVIKO-19, ambalo limeathiri dunia nzima na si Tanzania tu. Tangu janga hilo limeshuka nchini takriban miaka miwili iliyopita, hata mataifa makubwa yametikisika mno kiuchumi.

Ni kipindi ambacho hakukuwa na uzalishaji. Ni kipindi ambacho Serikali nyingi hasa za mataifa ya nje, yaliwafungia wananchi wao wasitoke, hivyo wengi hawakuwa wanakwenda kazini.

"Hakukuwa na uzalishaji, uzalishaji ndiyo unaanza sasa." Alisema Rais Samia.

Pili ni kwamba, hata baada ya hali kuanza kuwa nzuri, baadhi ya makampuni yakapunguza wafanyakazi kwa sababu tayari yalikuwa hayapo vizuri kiuchumi kwa kukosa kuzalisha kwa muda mrefu. Hilo pia lilisababisha hata kile ambacho kilitakiwa kizalishwe kwa idadi ya mwanzo, kilipungua kwa sababu ya uhaba wa wafanyakazi na uchumi pia.

Kwa maana hiyo mahitaji yanakuwa makubwa kuliko bidhaa zenyewe.

Hapo moja kwa moja ni lazima bidhaa zipande. Ndiyo maana Rais akaongea maneno haya.

"Kwa maana hiyo kama bidhaa ni chache duniani, bila shaka bei zitapanda." Alisema.

Rais alizungumzia upandaji wa mafuta. Akasema yamekuwa yakipanda, lakini pamoja na hayo serikali ilipunguza tozo ili kushusha bei ya mafuta kwa wananchi, lakini bado yamekuwa yakipanda, hivyo serikali imelazimika kurejesha tozo na kuwataka Mawaziri na Wabunge na wanaosimamia sekta, waambie wananchi ukweli.

Akasema vita ya Urusi na Ukraine imepandisha sana bei ya mafuta na yanapopanda kila kitu, nauli na usafirishaji wa bidhaa itapanda.

"Kwa hiyo waambieni wananchi ukweli, wasikae tu kulaumu serikali bei za mafuta zinapanda serikali haisemi kitu."

Hapa hakuna ujanja. Mafuta yakipanda, ina maana kila kitu ni lazima kipande. Kwa sababu vitu vyote vinasafirishwa kutoka eneo moja kwenda lingine. Achilia mbali kutoka nchi za nje na kuja hapa nchini.

Mafuta yanapopanda kwenye soko la dunia moja kwa moja huathiri kila kitu, ikiwemo upandaji wa bidhaa mbalimbali ikiwemo vyakula, na hii si Tanzania tu, bali kote duniani.

Inawezekana ikawa si bei za kudumu kwani bidhaa zitakapozalishwa nyingi kama zile zilizokuwepo kabla ya COVID-19, na vita ikaisha, inawezekana bei ikapungua, lakini kwa sasa tukubaliane na ukweli jinsi ulivyo kwa sababu hili ni la dunia nzima na si la hapa nchini tu.

Kwa Wabunge, Mawaziri na Wasimamia sekta ni wakati wa kuongea taratibu tu na wananchi na wakawaelewa. Watanzania ni wasikivu, wakikaa nao na kuwaambia sababu ya yote haya, watawaelewa.

Pia baadhi ya Watanzania ambao walikuwa hawaelewi ni kwa nini mafuta yamepanda na baadhi ya bidhaa kwa hotuba ya Rais, sidhani kama kutakuwa na maswali. Kila kitu kimeeleweka, inabidi tu tuombee uzalishaji uwe mkubwa na vita iishe, mambo yanaweza kuwa mazuri baadaye.

Nadhani kwa hili sitegemei tena kusikia malalamiko, badala yake Watanzania tuendelee kufanya kazi na kuzalisha mali. Kila kitu kimeeleweka, yoyote atakayeendelea kulalamika, basi ana lake jambo.

HABARI KITAIFA

# Umbali bado ni kikwazo watoto Vigwaza kusoma

**Na Julieth Mkireri,** VIGWAZA

TATIZO la wanafunzi kukatiza masomo katika kijiji cha Buyuni limeendelea kuelezwa kuwa kikwazo cha maendeleo katika vitongoji vya Kwedihungo na Kingubwi Kata ya Vigwaza wilaya ya Chalinze mkoani Pwani.

Wakizungumza na Nipashe jana baadhi ya wakazi wa vitongoji hivyo walisema shule iliyopo ipo mbali, hivyo wanafunzi hushindwa kumudu kutembea umbali wa kilomita saba hadi nane.

Zungu Landaiya, mmoja wananchi ambao wameelezea kero hiyo kwa wanafunzi ambayo imekuwa ikichangia baadhi yao kuwa watoro.

"Alisema kwa sasa wanafunzi wanasoma katika Shule ya Msingi Buyuni ambayo iko mbali na wanapoishi, pia shule ina uhaba wa vyumba vya madarasa kwani ina wanafunzi zaidi ya 700 huku ikiwa na vyumba vinne na walimu saba," alisema.

Marlian Ismail alisema wanafunzi wanaotoka katika vitongoji vya Kudihungo na Kingubwi wanalazimika kufika shuleni saa tatu asubuhi wakati wengine wakiwa wameshaanza masomo.

Ismail alisema wanafunzi hao wakati wa kurudi nyumbani wanafika saa moja jioni wakiwa wamechoka, hali inayosababisha wengine kushindwa kuendelea na masomo na pia kuwa na ufaulu hafifu.

Hariri Idd alisema katika kitongoji chao wameanza mpango wa kutafuta eneo kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa darasa la awali.

Alisema wanatarajia kuanza utekelezaji wa mpango huo kwani wanafunzi wadogo wanashindwa kuhilimili kutembea umbali huo na hata wengine wenye umri mkubwa wapo wanaokatisha masomo yao.

Wameiomba Serikali kusaidia kujenga shule karibu na vitongoji hivyo kuwawezesha watoto wanaoishi katika maeneo yao kupata elimu.

Hivi karibuni Idara ya Elimu Halmashauri ya Chalinze ilieleza mpango wake wa kutenga bajeti kwa ajili ya kutatua tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa kwenye shule hiyo kuondoa msongamano kwa wanafunzi.

# Kitila aishauri TANESCO kupunguza bei ya umeme

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEKUWA Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ameishauri Shirika la Umeme nchini (TANESCO) kuangalia uwezekano wa kushusha gharama ili wananchi waweze kuutumia umeme huo kwa matumizi yote badala ya taa peke yake.

Alitoa ushauri huo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa kuwasilishwa ripoti iliyofanywa na Taasisi ya Afya ya Ifakara kuhusu matokeo ya tathmini ya ukuaji wa majiji ya Dar es Salaam na Dodoma ikilinganishwa na upatikanji wa huduma za elimu na afya.

Alisema ripoti hiyo inaonyesha wananchi wanatumia umeme kwa asilimia 1.2, hivyo Watanzania wengi hasa wa mkoa wa Dar es Salaam matumizi ya umeme kwao ni kwa ajili ya mwanga.

Alisema inaonyesha bado gharama ya umeme ni kubwa ndio maana wananchi wanakimbilia kwenye matumizi ya gesi.

Prof. Kitila alisema TANESCO kuna haja ya kuangalia ili kushusha bei kuwawezesha wananchi wengi watumie umeme kwa matumizi mengine badala ya taa pekee.

Alisema eneo jingine ni matumizi ya gesi ambao ni asilimia 50 ya wakazi wa Dar es Salaam wanatumia gesi kama chanzo kikuu cha kupikia.

"Hili ni jambo kubwa kama Dar es Salaam inatumia asilimia 50 na asilimia 43 wanatumia mkaa ni jambo nzuri la kupongeza kwamba wakazi wa Dar es Salaam wanatumia gesi na asilimia 1.2 wanatumia umeme... hii ina maana kuwa wananchi wameona nishati ya gesi ndio njia sahihi ya kutumia," alisema.

Alisema kuna haja serikali kuongeza nguvu katika gesi kwani Watanzania wengi watatumia nishati hiyo.

"Watanzania wengi wakipatiwa nishati mbadala wanaweza kuitumia badala ya kuendelea kutumia kuni ama mkaa kwa jiji la Dar es Salaam kutumia mkaa kwa asilimia 43 ni kubwa ...kuna haja ya kuliangalia tulitegemea kutumia zaidi nishati mbadala ili kulinda maeneo ya mazingira yetu," alisema. Alisema lengo la utafiti ni kupokea matokeo ya mradi wa tathmini ya hali ya maeneo endelevu katika Jiji la Dar es Salaam hasa kwa kuzingatia sekta ya afya, elimu na ukuaji wa jiji kwa ujumla.

Alisema utafiti huo una matokeo mazuri kwa kuwa wameonyesha eneo la maji wamepiga hatua katika usambazaji wa majisafi na salama kuwa wananchi wanapata maji kutoka mfumo rasmi.

Alisema kwa upande wa maji kuna jambo la kufanyia kazi kwani utafiti huo unaonyesha asilimia tano ya wakazi wa Dar es Salaam wanatumia mfumo rasmi wa majitaka.

Alisema walio wengi wanajihangaikia wenyewe, hivyo kuna kazi kubwa upande wa serikali na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kufanyia kazi eneo la maji taka kwa kuwa ni changamoto kubwa.

Aidha, alisema katika ripoti hiyo imeonyesha kuna hatua kubwa ya elimu imefanywa katika uandikishwaji wa watoto shuleni kwa shule za msingi na sekondari.

Naye Msimamizi wa mradi na mtafiti kutoka Taasisi ya Afya Ifakara, Dk. Francis Levira, alisema kikubwa walichokifanya katika utafiti huo ni kupitia sera, ukuaji wa miji na kufanya sensa ya kaya.

"Tulichokikuta kuna masuala mengi ambayo tumepiga hatua kubwa kwenye usambazaji maji, elimu kwenye elimu ya shule ya msingi na sekondari na ufaulu mkubwa," alisema.



Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) mkoa wa Pwani, Alban Kihulla (wapili kulia), akifafanua jambo kuhusu utendaji kazi wa Kituo cha Misugusugu kwa Waziri wa Biashara na Maendeleo Zanzibar, Omar Said Shaaban (kulia), alipokitembelea mkoani humo, jana. Kushoto ni Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Exaud Kigahe na Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stela Kahwa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Uwekezaji machinjio ya kisasa walikuna Bunge

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, imeridhishwa na uwekezaji unaoendelea wa mradi wa fedha za serikali kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Mashirika ya Umma (PSSSF) kwenye Kiwanda cha Nyama cha Nguru Hills Ranch Limited kilichoko Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, alitoa kauli hiyo baada ya kamati hiyo kutembelea kiwanda hicho na kujionea shughuli mbalimbali zinazoendelea kufanywa za ujenzi wake ambao kinatarajiwa kuanza hivi karibuni.

Silaa alisema kamati hiyo imeridhishwa baada ya kuona fedha zilizowekwa na serikali kupitia PSSSF zinaonekana thamani yake na kuna matumaini makubwa fedha zilizowekezwa zitarudi baada ya muda mfupi.

Alisema Kamati imejionea bila shaka kuwa fedha zilizowekezwa Dola milioni 15 kwenye kiwanda kikubwa cha kisasa cha nyama zimewekezwa kwenye tija na kiwanda kitakachokuwa cha mfano nchini.

"Kamati ya Bunge imeridhishwa kwa uwekezaji huu utakapokamilika utasaidia walaji wa nyama na upatikanaji wa ngozi zenye ubora nchini," alisema Silaa.

Hata hivyo, aliiagiza Bodi ya Udhamini ya PSSSF kuhakikisha inaendelea kusimamia mkataba wa uwekezaji kwa kushirikiana na wabia wenzake, kwa lengo la kuhakikisha uzalishaji unaanza haraka ili kupata tija.

Agizo lingine kwa PSSSF ni kuongeza kipengele katika makubaliano yao na mwekezaji mwenza ambao ni Kiwanda cha Nguru Hills Limited kiwauzie ngozi Kiwanda cha Ngozi cha Kilimanjaro ambacho PSSSF imewekeza ili kipate malighafi za kuendesha.

Agizo lingine ni PSSSF na wawekezaji wenza kuanzisha programu maalum kwa wafugaji ili kuwe na mifumo maalum itakayokidhi kupata viwango vya mifugo vinavyokubalika katika kiwanda hicho.

Awali akitoa taarifa kwa kamati hiyo kuhusu Kiwanda cha Machinjio ya kisasa, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema kitakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku.

Alisema mradi huo wa machinjio hayo ya kisasa yanamilikiwa kwa ubia wa wanahisa watatu kati ya serikali kupitia PSSSF, Eclipse Investment (LLC) na Kampuni ya Busara Investment (LLP).

# UNFPA yakoleza moto vita ya UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Afya ya Uzazi na Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, limesema, kupata chanjo ya UVIKO-19 ni jambo muhimu kuanzia kwa mtu binafsi, familia na jamii kwa ujumla.

Meneja Mawasiliano wa shirika hilo, Warren Bright, alisema mtu anapopata chanjo, anakuwa amepunguza kasi ya ugonjwa huo na pia atakuwa ameweka ulinzi kwake, kwa familia na jamii inayomzunguka.

Kutokana na umuhimu huo, alisema karibu wafanyakazi wote wa shirika hilo na wategemezi wao wameshachanjwa na kwamba wanafuata miongozo yote ya wataalamu wa afya ya kudhibiti ugonjwa huo.

"Yaani ni kwamba, wafanyakazi waliochanjwa, hakuna aliyelazimishwa, kila mmoja amechanjwa kwa hiari yake, kwa kuwa wanajua umuhimu wa kupata kinga dhidi ya ugonjwa huo," alisema Bright-on.

Alisema elimu ya chanjo inaendelea kutolewa ili kuhakikisha kila mtu anapata taarifa sahihi kwa wakati na kumwezesha kuchukua hatua za kulinda afya yake kwa hiari.

"Binafsi ninaona chanjo imesaidia kuniepusha na magonjwa nyemelezi yanayosababishwa na mzio kama mafua, kuumwa kichwa mara kwa mara, kwani kwangu hayo yametoweka," alisema Bright.

Alisema alipochanja, chanjo haikumpa usumbufu wowote na kwamba anaendelea na shughuli zake kama kawaida, kinyume na baadhi ya watu ambao wamekuwa wakiaminisha jamii kuwa chanjo hiyo si salama.

Bright alisema suala la chanjo ya UVIKO-19 lina uzito wake, na kwamba uzito huo ndiyo ambao umechangia wafanyakazi wa shirika hilo kujitokeza kwa wingi kuchanja pamoja na familia zao

"UNFPA hufuata sera ya kushirikiana na nchi husika kupanga mahitaji muhimu ya nchi hiyo na hapa nchini, inazingatia maeneo matatu muhimu, afya ya uzazi, suala la jinsia hasa kwa kuongeza uwezo wa kinamama kufanya maamuzi, na la tatu likiwa ni idadi ya watu na maendeleo," alisema.

Alisema shirika hilo linaunga mkono juhudi zote zinazofanywa na serikali za kukabiliana na UVIKO-19 kwa kutoa hamasa na elimu ili jamii ipate taarifa sahihi za ugonjwa na kujitokeza kuchanja.




Ofisa Mtedaji Mkuu wa Taasisi ya Southern Africa Embrace Foundation, Dk. Sindy Zemura-Bernard, akizungumza kwenye kongamano la Women Lead Forum, lililoandaliwa na taasisi hiyo jijini Dar Es Salaam mapema wiki hii, kwa ajili ya kuhamasisha viongozi wanawake katika jamii ili kuleta mafanikio endelevu ya kiuchumi na kujenga usawa wa jinsia nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAWA yageukia kukuza utalii hifadhi changa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA), imetumia zaidi ya Sh. bilioni moja kujenga miundombinu kwenye Pori la Akiba la Swagaswaga ukiwa mkakati wa kukuza utalii kwenye hifadhi changa.

Meneja wa Pori la Swagaswaga, Joseph Reuben, altoa kauli hiyo alipokuwa akitoa wasilisho kwa wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii walipofanya ziara ya kukagua miradi iliyotekelezwa na TAWA.

Reuben, alisema awali watumishi 38 wa pori hilo walikuwa na makazi yao Dodoma Mjini, lakini kupitia mradi wa nyumba za watumishi uliogharimu Sh. milioni 334, watumishi wanne wanaishi eneo la hifadhi kwa ajili ya kutoa huduma.

"TAWA imetekeleza miradi ya maendeleo ya miundombinu ya maji, bweni la wageni wanaotembelea hifadhini, jengo la ofisi, ghala la kutunzia silaha na nyumba nne za watumishi," alisema.

Aidha, katika mradi mwingine mamlaka hiyo imejenga bweni la kupumzikia wageni lenye vyumba 18 liligharimu Sh. milioni 344.

Alisema kutokana na Pori la Swagaswaga kupakana na vijiji vya Chemba, Kondoa na Wilaya ya Hanang', kumekuwa na uvamizi wa wanyamapori wakali na waharibifu, hivyo kulifanya pori kuelimisha jamii jinsi ya kujilinda na wanyamapori hao.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2021 walidhibiti matukio ya uvamizi wa wanyamapori 84 na kuwaua fisi wawili ambao walijeruhi watu wanane.

Kaimu Kamishna wa TAWA, Mabula Nyanda, aliiomba Kamati ya Bunge kuwaongezea bajeti ili watekeleze miradi ya miundombinu kwenye mapori machanga kama Swagaswaga. Alisema hifadhi nyingi nchini zina changamoto ya miundombinu ya barabara na kuifanya mamlaka hiyo kutumia Sh. bilioni tisa kati ya 12.9 ambazo hutolewa kupitia bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuboresha miundombinu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Ally Makoa, aliwataka askari wa hifadhi hiyo kudumisha mahusiano mazuri na wananchi.

Makoa alisema hifadhi nyingi zina changamoto ya uwapo wa migogoro kati ya mamlaka za hifadhi na wananchi hususani katika kugombea ardhi, hivyo waendelee kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa uhifadhi na kujua mipaka yao.

"Kidogo katika suala la uhusiano mmeanza vizuri hasa kwa mpaka wa Chemba, lakini kwa upande wa Kondoa bado nimesikia kuna mgogoro, ila kwa ninavyowaona mnaingiliana na wananchi, hivyo mmejitahidi," alisema.

## Matatani kwa madai ya kumlawiti mtoto

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba linamshikilia Jabu Hamad Shehe (35), mkazi wa Kiuyu Changa kwa tuhuma za kumlawiti mtoto wa kiume (13).

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Juma Sadi Khamis, alisema kuwa, tukio hilo lilitokea kijiji cha Kiuyu Kimbo Machi 17, mwaka huu majira ya asubuhi.

Alisema mtuhumiwa huyo anaendelea kushikiliwa, na upelelezi utakapokamilika atafikishwa mahakamani.

"Tukio hilo likiripotiwa kituo cha Polisi Mchangamdogo Wilaya ya Wete na baadaye mtoto alipelekwa Hospitali ya Wete kwa uchunguzi, na ilikundulika kwamba ameshaharibiwa katika sehemu yake ya siri ya nyuma," alisema.

Kamanda Sadi alisema kutokana na kuibuka kwa kasi matukio ya ulawiti katika jamii, ni vyema kwa wazazi wawafuatilie watoto wao hatua kwa hatua, kwani athari yao ni kubwa.

"Mtoto akilawitiwa mwisho wake inakosekana ile hadhi yake ya kuwa mwanaume na pia tunakosa vijana wenye nguvu ya kufanya kazi katika kulisogeza taifa mbele kimaendeleo, hivyo jitihada zinahitajika kudhibiti hali hii," alisema.

Aidha, aliitaka jamii kutoa elimu kwa watoto wao ili wasijiingize katika matendo hayo machafu na yeyote atakayejaribu kufanya vitendo hivyo, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

**"Tukio hilo likiripotiwa kituo cha Polisi Mchangamdogo Wilaya ya Wete na baadaye mtoto alipelekwa Hospitali ya Wete kwa uchunguzi, na ilikundulika kwamba ameshaharibiwa katika sehemu yake ya siri ya nyuma," alisema.**

HABARI KITAIFA

# CUF, TLP zilivyopata hati za shaka, chafu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Wananchi (CUF), kimetajwa kuwa miongoni mwa vyama vitatu vya siasa vilivyopata hati yenye shaka katika ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21.

CAG, Charles Kichere alisema juzi alipokuwa akiwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kwa Rais Samia Suluhu Hassan, na kwamba katika ukaguzi wake kwa upande wa vyama vya siasa, vinne vimepata hati mbaya, vitatu hati yenye mashaka na viwili walishindwa kutoa maoni.

Alisema vyama vya CUF, UDP, SAU vilipata hati zenye shaka huku vilivyopata hati mbaya katika ukaguzi huo ni ADC, Chaumma, UMD na TLP na Chama cha Demokrasia Makini na AFP walishindwa kutoa maoni katika ukaguzi huo.

Awali, alisema hati 970 kati ya 999 zilizotolewa zinaridhisha, huku zenye shaka ni 19 na mbaya ni sita.

"Nilitoa hati nne za kushindwa kutoa maoni sawa asilimia 0.4, ukilinganisha na mwaka jana kuna ongezeko la hati safi na kupungua kwa hati zenye shaka, mbaya na za kushindwa kutoa maoni," alisema.

Alitaja taasisi zilizopata hati zenye shaka, mbaya na kushindwa kutoa maoni ni Jiji la zamani la Dar es Salaam, Halmashauri za Wilaya ya Kisarawe (Pwani), Longido (Arusha), Mlele (Rukwa), Musoma (Mara), Sengerema (Mwanza) na Bunda (Mara).

Kwa upande wa mashirika ya umma, taasisi zilizopata hati yenye shaka ni Mamlaka ya Maji na Ustawi wa Mazingira Geita, Muleba, Ngara (Kagera), Tabora, Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Mamlaka ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Nyingine ni Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN).

Pia alisema Shirika la Masoko Kariakoo na Shirika la Reli Tanzania walishindwa kutoa maoni katika ukaguzi huo. Kwa upande wa Serikali Kuu, alisema Jumuiya ya Tawala za Mikoa (ALAT), Baraza la Madaktari Tanganyika zilipata hati yenye shaka.




Meneja Biashara wa Tigo Pesa, Fabian Felician, akizungumza wakati wa uzinduzi wa bahati nasibu kupitia simu ya mkononi iitwayo 'Dilipesa', kwa ushirikiano na kampuni za Dunia Investment na Axieva, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadaiwa kukutwa na nyara za serikali

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wanne kutoka Wilaya ya Nachingwea katika mikoa ya Lindi na Dar es Salaam wanashikiliwa kwa mahojiano na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumiliki silaha na kilo 69,261 za nyara za serikali kinyume cha sheria.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Mtatiro Kitinkwi, alitoa kauli hiyo alipokuwa anatoa taarifa ya utekelezaji kwa waandishi wa habari, huku akiwasisitiza kutowataja majina kutokana na alichokieleza ni kupewa maelekezo na mamlaka za juu.

Kamanda huyo alisema watuhumiwa walikamatwa Machi 17, mwaka huu, kufuatia msako uliofanywa na askari polisi kwa kushirikiana na wa uhifadhi.

Alisema katika msako huo wa kudhibiti vitendo vya ujangili, watuhumiwa wanadaiwa kukamatwa na kilogramu 261 za nyama na mkonga mmoja wa meno manne ya tembo yenye thamani ya Sh. 69,510,000.

Vingine ni bunduki moja aina ya Rifle 375, maganda saba na vichwa sita vya risasi, ikiwamo moja iliyotengenezwa kienyeji na mitego ya waya (roda) iliyokuwa inatumiwa na watuhumiwa hao, huku akieleza kuwa nyama waliyoikamata imechomwa moto kwa mujibu wa taratibu.

"Hiki kielelezo cha nyama kimechomwa moto kwani ni kitu kisichostahimili kukaa kwa muda mrefu hadi kesi itakapoisha," alisema Kitinkwi.

Kitinkwi alisema katika mahojiano ya awali watuhumiwa walikiri kufanya mauaji ya tembo katika mapori ya wazi ya Nyera, Kipelele (TFS) na (Hingai) kwenye kijiji kilichopo Kata ya Kiangara, Wilaya ya Liwale.

Kamanda huyo alisema watuhumiwa wanaendelea kushikiliwa kwa uchunguzi wa kina na utakapokamilika watafikishwa mahakamani.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na serikali kwa kutoa taarifa kwa jeshi hilo wanapobaini vitendo vya uhalifu.

## Mil. 300/- za UVIKO kuboresha huduma za maji wilayani Musoma

**Na Sabato Kasika**

WILAYA ya Musoma mkoani Mara, imepata Sh. milioni 300 za UVIKO-19, kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji kwenye baadhi ya vijiji kusogeza huduma hiyo muhimu karibu na wananchi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Wakala wa Huduma za Maji Mjini na Vijijini (RUWASA), wa wilaya hiyo, Mhandisi Edward Silonga, alitaja vijiji vitakavyofaidika na fedha hizo ni Nyasaungu Kata ya Ifulifu na Kurwaki Kata ya Mugango.

"Serikali imetoa Sh. milioni 600 kupitia mradi wa bomba la maji wa Mugango hadi Butiama unaopitia Kiabakari, ili kusambaza maji kwenye baadhi ya vijiji vya wilaya hizi mbili za Musoma na Butiama," alisema Silonga.

Alifafanua kuwa katika mgawo huo, kila halmashauri imepata Sh. milioni 300 na kwamba tayari kwa upande wa wilaya yake, mafundi wapo kwenye vijiji hivyo ili kufanya kazi ya kusambaza mabomba ya maji.

Baadhi ya miradi hiyo ni Kijiji cha Suguti kilichoko kando ya Ziwa Victoria kuelekea vijiji vya Chororwe, Nyambono, Saragana hadi Bugoji ambako mabomba yameshatandikwa.

Alisema wameshaweka tangi kubwa lenye uwezo wa kuchukua lita 200,000 za maji na kuyasambaza katika vijiji vya Saragana, Nyambono na Bugoji ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi.

Alisema serikali ilishatoa zaidi ya Sh. bilioni 8 kutekeleza miradi ya maji katika vijiji mbalimbali vya wilaya hiyo, vikiwamo baadhi ambavyo tayari vimeanza kupata huduma hiyo.

"Kwa mfano, Kata ya Suguti kuna mradi wa maji umefikisha huduma hiyo kwa wananchi majumbani, lakini yapo maeneo hayajaipata kutokana na changamoto ya kupitisha mabomba barabarani," alisema.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo, aliishukuru serikali kwa jitihada za kuhakikisha huduma ya maji inapatikana umbali mfupi.

Alisema utekelezwaji wa miradi ya maendeleo jimboni humo unatokana na ushirikiano kati ya wananchi, viongozi wao akiwamo yeye, wakichangia nguvukazi na fedha taslimu, huku serikali nayo ikiwaunga mkono.

# Wawekezaji katika sekta utalii wahakikishiwa mazingira wezeshi

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amesema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa sekta ya utalii, pamoja na kuendelea kuboresha huduma za kitalii.

Amesema serikali pia itawezesha upatikanaji wa leseni ya shughuli za utalii kwa uharaka zaidi pamoja na mifumo ya malazi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akikabidhi vyeti kwa wawekezaji waliokidhi vigezo na kufanikiwa kupata maeneo ya uwekezaji mahiri katika maeneo ya wanyamapori (SWICA), yanayosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Kampuni zilizokabidhiwa vyeti hivyo ni Grumet Services Ltd pamoja na Mwiba Holding LTD.

Dk. Ndumbaro alisema Wizara ya Maliasili na Utalii itaendelea kutoa fursa katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa wawekezaji wa ndani na nje kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi.

Hivyo, aliwasisitiza wawekezaji wazawa pamoja na wa kigeni kulinda na kutangaza utalii na maeneo ya uhifadhi na vivutio hapa nchini, katika maeneo waliyopewa kuwekeza kwa kushirikiana na serikali.

Aidha, Waziri Ndumbaro alitumia fursa hiyo kuwahamasisha wawekezaji wa kigeni kuwekeza nchini, akitaja Tanzania kuwa ni salama, yenye amani na demokrasia.

"Wizara ya Maliasili na Utalii, falsafa yetu ni moja tu, mteja ni mfalme. Ndiyo maana mimi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, tuko tayari kukutana na mwekezaji wa aina yoyote yule, muda wowote ule kujadili changamoto zozote zile, milango iko wazi," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TAWA, Meja Jenerali Mstaafu, Hamis Semfuko, aliishukuru Serikali na Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kuipatia TAWA Sh. billioni 12.9, ili kutekeleza miradi ya miundombinu ya utalii.

Alisema miradi hiyo inaendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali, huku akithibitisha kuwa TAWA imeweka mipango madhuhuti kuhakikisha miradi yote ambayo imekusudiwa kutekelezwa kwa kutumia fedha hizo inatekelezwa ndani ya muda uliopangwa na kwa ubora uliokusudiwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Grumeti Reserves Ltd, Graham Ledger, alishukuru kwa kupewa cheti cha umiliki wa vitalu viwili, aliahidi kushirikiana na Serikali katika kulinda na kuendeleza shughuli za uhifadhi nchini.



Washindi mbalimbali waliojishindia zawadi za Tv za kisasa na simujanja kwenye promosheni ya Vodacom ya Shangwe Lipo Pale Pale kutoka mkoani Songwe, wakiwa kwenye picha ya pamoja na Meneja Mauzo wa Vodacom wa mkoa huo, Humphrey Mutabiirwa (wanne kulia), baada ya kuwakabidhi zawadi zao, katika stendi kuu ya Mwaka mjini Tunduma mapema wiki hii.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamishna Bima 'azing'ata' sikio benki

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware, amezitaka benki na taasisi za kifedha kuzitumia fursa lukuki zilizoko kwenye sekta bima ili kuleta matokea chanya kwa ukuaji na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Benki na taasisi za kifedha mpo katika nafasi nzuri ya kuchagiza ukuaji na maendeleo ya uchumi wa Tanzania kupitia huduma na bidhaa za bima. Kama TIRA tumejipanga kufanya kazi kwa karibu sana na benki," Dk. Saqware alisema.

Akizungumza katika ziara yake ya kwanza kutembelea Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam jana, Dk. Saqware mbali ya kuipongeza benki hiyo kwa kujipanua zaidi, alisema TIRA imekuja na mkakati wa kuhakikisha kuwa huduma na bidhaa za bima zinawafikia wadau na kuongeza mchango stahiki kwenye soko sambamba na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Alisema TIRA kama msimamizi mkuu wa shughuli za bima nchini, amewaahidi wadau katika sekta ya bima kuendelea kuwapo kwa mazingira mazuri ya kufanya kazi ikiwamo marekebisho ya sheria na kanuni itakapohitajika.

"Ni vizuri mnapoona kuna sababu ya msingi ya kufanyia marekebisho kanuni fulani basi leteni mapendekezo yenu ili yafanyiwe kazi. Sisi (TIRA) tupo kwa ajili ya kuleta ufanisi na kuongeza ustawi pamoja na ukuaji wa sekta ya bima," alisema.

Aidha, Dk. Saqware alipongeza Benki ya CRDB kwa kuweka kipaumbele chake kuchangia maendeleo ya sekta ya kilimo kwa kuja na mpango wa kuanzisha bima ya kilimo kwani itatoa msukumo mkubwa.

Alisema elimu zaidi kuhusu huduma na bidhaa za bima inapaswa kutolewa zaidi kwa Watanzania ili waweze kunufaika nazo, na kwamba TIRA imejipanga kuendelea kutoa kuhusu umuhimu na faida za kutumia huduma za bima.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, AbdulMagid Nsekela, alizungumzia umuhimu wa kurejeshwa kwa 'Direct Sales Force or Representative ili kupanua na kuongeza wigo wa ajira kwa vijana.

"Huu utaratibu ukirudishwa utasaidia sana kuongeza zaidi ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu katika eneo la bima, mpango huu utatoa fursa nyingi kwa wahitimu wetu na kuchangia ukuaji wa sekta hii muhimu," alisema Nsekela.

Alimshukuru Kamishna wa Bima kwa kuitembelea benki yake na kufanya mazungumzo na menejimenti na alimwahidi kuendelea kushirikiana na kufanya kazi kwa karibu na TIRA.

## TBL yaalika kampuni chipukizi kujiunga na Accelerator 100+

**Na Mwandishi WETU**

KAMPUNI ya Tanzania Breweries Limited (TBL) inayomilikiwa na kampuni ya AB InBev, imetoa wito kwa wavumbuzi kutoka mikoa yote nchini kutuma maombi ya kujiunga na programu ijulikanayo kama 100+ Accelerator ili kuchangia katika kutafuta suluhisho la vikwazo vya maendeleo endelevu.

Programu ya 100+ Accelerator iliyoanzishwa mwaka 2018, imefanya kazi nyingi ikishirikiana na kampuni kubwa duniani kutafuta suluhisho la vikwazo vya ugavi, utunzaji maji, kilimo endelevu, mabadiliko ya tabianchi, ukuaji wa pamoja na viumbe hai.

Mwaka huu programu hii imelenga kutafuta suluhisho la kivumbuzi litakalokuwa kwa haraka na kuleta mabadilko makubwa kwenye maeneo yenye vikwazo.

Programu ya 100+ Accelerator imekuwa ikijikita kufanya kazi na kampuni ndogo chipukizi ambazo tayari zilikuwa na bidhaa sokoni au zinazokaribia kwenda sokoni.

Vilevile, programu hiyo inalenga kuwezesha kampuni zinazoongozwa na wajasiriamali wenye shauku na wenye ukaribu na watu wa aina mbalimbali wenye ujuzi na wenye nafasi kubwa ya kufanikiwa.

"Sasa tumeanza rasmi kupokea maombi ya msimu wa nne wa Accelerator 100+, programu ya kimataifa kwa udhamini wa AB InBev na mashirika washiriki.

"Accelerator 100+ inafanya kazi na kampuni chipukizi kupata suluhisho endelevu la changamoto za dunia zinazohusiana na maji, uchumi endelevu, mabadiliko ya tabianchi, kilimo, ukuaji wa pamoja na viumbe hai.

"Baada ya kuchaguliwa, washiriki watapata ushauri, mafunzo na kiasi cha pesa dola za kimarekani 100,000 zitakazowasaidia kutekeleza miradi yao ya majaribio kwa kushirikiana na baadhi ya chapa pendwa duniani," alisema Abigail Mutoboyerwa, Meneja wa Masuala Endelevu TBL.

Kwa miaka miwili iliyopita, programu hiyo imeongezea uwezo kwa kampuni 70 kwenye nchi zaidi ya 20. Programu ya 100+ Accelerator inatumika kuwaongeza uwezo wajasiriamali wenye shauku kwa kuwasaidia kuleta bidhaa zao sokoni haraka.

Alisema kampuni hizi zinazochipukia zimefanikisha kuleta zaidi ya dola za kimarekani milioni 300 na zinaendelea kukua kwenye ngazi ya kimataifa ili kufikia malengo ya programu, kuongeza kasi ya kuipeleka dunia kwenye kutumia suluhisho endelevu na kufanya biashara kwa njia sahihi na si njia rahisi.

"Tumeona kazi iliyofanywa na 100+ Accelerator kusaidia wajasiriamali wenye shauku ya kutafuta suluhisho za changamoto za kimataifa na kusaidia kuleta suluhisho zao sokoni haraka.

"Ushirikiano huu ni nafasi ya kujumuika pamoja katika kuongeza kasi ya kupata ulimwengu endelevu zaidi wakati kila kampuni ikiendelea kujitahidi kufikia malengo yake ya kuwa endelevu," alisema Mkurugenzi wa TBL, Jose Moran.

Ukurasa 13




Kupanda kwa cheo chako si mwisho wa majukumu



Ulanguzi wa sukari Moshi wamwinua kitini RC kumsaka anayemchezea

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA APRILI 1, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Uungwana wao Unguja wawafanya watalii Ukraine hawataki kuondoka

- Wakataa ofa Ulaya, wahamia Uswahilini
- Wenye weledi wa IT waendeleza kazi zao

NI mwezi mmoja sasa na siku kadhaa tangu kuanza kwa vita kati ya Russia na Ukraine, dunia ikiendelea kushuhudia athari kutokana na mgogoro huo.

Rais Samia Suluhu Hassan, juzi tu alitangaza kuwa imekuwa chanzo cha gharama ya juu ya bidhaa nchini, kati ya sababu tatu alizotoa.

Baada ya kuanza vita hivyo mwezi jana, Zanzibar ilijikuta ina watalii kutoka nchini Ukraine wapatao 1000 wakiwa hawajui hatima yao ya kuwa ugenini na ile ya familia zao.

Hata hivyo, kutokana na jitihada mbalimbali, wengi wao hivi sasa wameondoka na kwenda kuanza maisha katika nchi nyingine kama vile Ufaransa, Ujerumani na Hispania na wapo walioamua kubaki Tanzania, licha ya kupata fursa za kwenda kuanza maisha katika nchi za Ulaya.

Sasa wanatetea uamuzi wao, wanajiona wako salama zaidi Zanzibar kuliko kwingineko duniani, hoja inayosikika kutoka kwa mtalii Olha, kutoka Ukraine, ambaye kwa mwezi mmoja sasa amejikuta amekwama na mwenzake baada ya kufika Zanzibar kufanya utalii.

Kabla ya vita kuanza walikuwa katika moja wa hoteli za kitalii, lakini baada ya vita tu kuanza, maisha yakabadilika. Fedha za matumizi zikawaishia, hali iliyowalazimu kubadilisha mfumo wa maisha kwenda kuishi sehemu za bei rahisi zaidi.



Watalii raia wa Ukraine waliokwama Unguja. **PICHA: MTANDAO.**

Hata hivyo, licha ya hivi sasa kupewa hifadhi ya bure katika mojawapo ya hoteli zinazomilikiwa na raia wa Ukraine, bado changamoto yao kubwa ni fedha za kujikimu kila siku.

Hivyo, kuna wakati wanategemea msaada wa chakula kutoka kwa wasamaria wema, hasa wenyeji wa Matemwe, Unguja.

Olha na mwenzake hivi karibuni walipata nafasi ya kwenda nchini Poland, lakini wakaikataa, wakisema wanajihisi wapo salama zaidi wakiwa Zanzibar.

"Tunajisikia tuko salama zaidi hapa. Tutakaa hapa mpaka vita vitakapokwisha, baada ya hapo tutaona nini cha kufanya. Tulipata nafasi ya kwenda Poland, lakini tuliamua kubaki hapa baada ya kuona raia wengi kutoka Ukraine wameingia Poland," anasema Olha.

Hii inaonekana kwa baadhi ya watalii wanaoendelea kujishughulisha na kazi za mitandaoni ili kujipatia kipato cha kuweza kujikimu kimaisha.

Ozirnyi Kyrylo, ni mfanyabiashara wa soko la hisa. Licha ya kukwama nchini Tanzania, lakini ameweza kutumia ujuzi wake kuendelea kufanya kazi kupitia mtandaoni.

Kipato chake, kimemsaidia kulipa kodi ya nyumba, pia kumtumia mama yake ambaye yuko ugenini fedha za kijikimu.

"Mimi ni mfanyabiashara wa soko la hisa. Kwangu mimi kitu muhimu ni kuwapo mtandao, ambao ninao hapa. Hii ni kama ofisi yangu, mara nyingine nafikiria kuhusu vita, lakini sasa hivi familia yangu iko sehemu salama, hivyo mara nyingi najikita katika kufanya kazi," anasema Ozirnyi Kyrylo.

Kadri vita vinavyoendelea, miundombinu nayo inazidi kuharibika huku kampuni na mashirika yakiendelea kuyumba na kuwa hatarini kusitisha shughuli zake nchini Ukraine. Hii inaondoa matumaini ya baadhi wanaofanya kazi kwa njia ya mtandaoni.

Ivanna Leibiuk, ambaye amekwama Zanzibar na binti yake Veronica mwenye umri wa miaka 12, yeye ni mtaalamu wa masuala ya teknolojia ya mawasiliano na amekuwa akiendelea na kazi yake kwa kutumia laptop. Hivi sasa amejawa na wasiwasi wa kupoteza kibarua ambacho ndio tegemeo lake.

"Nafanyakazi katika kampuni ya IT kupitia laptop yangu, lakini mambo hayatabiriki, nahofia kupoteza kazi yangu wakati wowote kwa sababu mambo hayataribiki kutokana na vita," anasema Ivanna Leibiuk.

Idadi kubwa wa watalii hawa hivi sasa wamehama katika hoteli za kitalii na kutafuta makazi ya muda uraiani, lakini hoteli nyingi za kitalii zimeendelea kuwa na msaada mkubwa kwao.

Gilbert Kazungu ni Meneja Mkuu wa hoteli ya Amani Beach Bungalow, anasema walikuwa mstari wa mbele kutoa kila aina ya msaada, ikiwemo kuwapa punguzo la chini kabisa baadhi ya watalii waliokwama.

"Tunajua kwamba, shida zinakwisha na hawa watalii iko siku watarudi Zanzibar kutokana na ukarimu wetu," anasema Gilbert Kazungu.

Hivi sasa, katika maeneo mengi ya utalii Zanzibar, kama vile Nungwi, Matemwe na hata Paje, baadhi ya wenyeji hivi sasa wao ndio wamekuwa msaada mkubwa kwa wageni wao.

Juma Abdallah ambaye ni 'Beach Boy' wa Nungwi, anasema hali ya baadhi ya wageni inasikitisha na kuna wakati analazimika kuwapelekea msaada wa chakula wageni wake.

Hivi sasa msimu wa utalii uko chini, hali inayowafanya baadhi ya watalii hawa waliokwama kuweza kuyamudu maisha katika eneo ambalo maisha yake ni ghali kutokana na kuendeshwa na shughuli za utalii.

- ***Kwa mujibu wa BBC.***

BIASHARA

# Ulanguzi wa sukari Moshi wamwinua kitini RC kumsaka anayemchezea

- Wazalishaji TPC wawasukumia wasambazaji
- Wakazi watoa siri, inafichwa kupandisha bei

**Na Mary Mosha, MOSHI**

KILIMO cha miwa kitaalamu kinaelezwa kuwa na tija na kinaweza kufanywa na mkulima yeyote, hata kuibua faida kubwa kiuchumi kwa pande zote, mtu binafsi, jumuiya yake na serikali kwa ujumla.

Pia, ulimaji miwa una msaada mkubwa kwa nchi katika uzalishaji sukari, ambayo ni hitaji muhimu kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya umma, iwe moja kwa moja au malighafi ya uzalishaji.

Hadi sasa Tanzania inakabiliwa na tatizo la upungufu wa uzalishaji sukari, hata serikali inalazimika kuagiza kutoka nje ya nchi, ili kuziba pengo lililoko.

Takwimu za Wizara ya Kilimo, zinaonyesha uzalishaji sukari nchini umekuwa ukiongezeka katika kipindi cha miaka mitano, kutoka tani 295,775 kwa mwaka 2015/2016 hadi tani 377,527 za ndani ya msimu wa uzalishaji 2020/2021.

Takwimu hizo za kitaifa zinaonyesha mahitaji ya sukari kitaifa yanakadiriwa kuwa tani 710,000, ambayo mgawanyo wake ni tani 545 kwa matumzi ya nyumbani na viwandani ni 165. Hata hivyo, Bodi ya Sukari inasema kiwango cha uzalishaji kinagota katika wastani wa tani 370,000 kukiwa na pengo la hitaji la tani 340,000.

Hata hivyo, kuna malalamiko ya kuwapo uzalishaji usioridhisha kwa wafanyabiashara kutokuwa waaminifu na kufanya urasimu wa kuificha kisha wanawauzia watu kwa bei ya juu na kusababishia umma hali ngumu.

Katika kutambua kuwapo pengo la uzalishaji sukari kitaifa, mkoa wa Kilimanjaro umekuja na mikakati kuwabana baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wanaotajwa kuwa chanzo cha kupanda bei ya sukari mkoani humo, wakinunua sukari viwandani na kuificha, wakilenga uhaba unaosababisha bei kupanda.

**RC ANAVYOKERWA**

Ni jambo linalotajwa kimkoa kuwa linachangia sababu ya bidhaa ya sukari kupanda bei katika maeneo mbalimbali mkoani Kilimanjaro, hujuma hiyo inamuibua Mkuu wa Mkoa, Steven Kagaigai, anayesema hatofumbia macho hujuma hiyo kwa wakazi wa mkoa huo.

Anawaonya wafanyabiashara wanaofanya hayo wabadilike haraka, akidodosa kuwa ameunda kikosi kazi maalum kuibua undani wa tatizo lilipo na kuyapatia majawabu sahihi ya kuondosha tatizo hilo la kupanda bei ya sukari kwa umma.



Uongozi wa serikali mkoani Kilimanjaro, ulipozuru kiwanda cha sukari TPC kupata ufafanuzi wa hali ya uzalishaji sukari. **PICHA: MARY MOSHA.**

> **"Kupanda kwa bei kiholela lazima tukomeshe. Nawaomba sana wafanyabiashara mnachofanya ni kosa kubwa, hivyo mnapaswa kubadilika na kufanya biashara kwa amani na utulivu," anasema.**

Kagaigai anasema, serikali imeridhishwa na uzalishaji wa sukari unaofanyika katika Kiwanda cha Sukari TPC kilichopo Moshi, uzalishaji wake ukiwa na tija kuanzia jamii inayowazunguka na taifa kwa ujumla.

"Nimeshuhudia huu uzalishaji uliofanyika hapa, lakini niwahakikishie serikali imeunda kikosi kazi maalumu kuchunguza tatizo hili ambalo linaonekana kuendekezwa na wafanyabiashara, ili mwishowe kuwe na suluhisho la kudumu," anasema.

Mkuu wa Mkoa anafafanua, matatizo ya uhaba wa sukari yamekuwa yakijirudia na sasa serikali imejipanga katika kuhakikisha jambo hilo linatoweka.

"Kupanda kwa bei kiholela lazima tukomeshe. Nawaomba sana wafanyabiashara mnachofanya ni kosa kubwa, hivyo mnapaswa kubadilika na kufanya biashara kwa amani na utulivu," anasema.



Shamba la miwa la kiwanda cha sukari TPC lililoko Moshi, ambayo ni malighafi yake. **PICHA: MTANDAO.**

**KIWANDANI TPC**

Kiwanda cha TPC kinaeleza hadi sasa kimeongeza uzalishaji wake wa sukari kutoka tani 108,000 zilizokuwa zikizalishwa kwa mwaka hadi kufikia tani 108,800 mwaka huu ikilinganishwa na uzalishaji wake msimu uliopita. Ni ziada ya uzalishaji tani 800 zilizoongezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu na Utawala wa Kiwanda hicho, Jafary Ally, anasema wao wana sukari ya kutosha kukidhi soko la mkoa, ila kinachotokea katika soko hilo ambako kunasambazwa na wengine wa mamlaka tofauti za kibiashara, hawafahamu undani wake.

Anasema kiwanda hicho kimeboresha uzalishaji wa sukari kutoka tani 36,000 kwa mwaka zilizokuwa zikizalishwa mwaka 2000 hadi tani 108,000 za mwaka uliopita.

Mtendaji Mkuu huyo, anaahidi iwapo miwa ikizalishwa kwa kiwango cha juu, kutoka tani 360,000 hadi tani milioni 1.1 kwa mwaka, watafanya mapinduzi ya uzalishaji.

Pia, Ally anaeleza wakati mwaka 2000 walichangia Pato la Taifa kwa Sh. bilioni mbili, sasa wamekwea hadi kuchangia zaidi ya Sh. bilioni 90, sehemu kubwa ikiwa ni katika kodi huku wakitoa gawio kwa serikali la Sh. bilioni 15 kila mwaka.

"Kwa miaka mitano iliyopita tangu mwaka 2017, Kiwanda cha Sukari cha TPC hakijawahi kupandisha bei kubwa ya sukari. Kuanzia mwaka 2017 hadi leo mwaka 2022, kiwango cha sukari kilichoongezeka katika bei ni Sh. 100 tu kwa kilo," anafafanua.

Kwa mujibu wa Jaffary, TPC inauza tani 450 za sukari kwa siku, lakini kwa kipindi kilichoko wamesimamisha uzalishaji kwa ajili ya ukarabati mitambo yao, wamejitokeza wafanyabiashara wengi na sasa kiwanda kinauza tani 600 za sukari kwa siku.

"Sisi TPC tumekuwa na utaratibu wetu ambapo kila mwaka huwa tunafunga kwa miezi mitatu ili kukarabati mitambo ya kiwanda chetu na wala hakuna kutengeneza uhaba wowote wa sukari na wanayo ya kutosha" anasema.

**WAKINENACHO WANANCHI**

Matilda Mfuru ni mkazi wa Manispaa ya Moshi, anasema wafanyabiashara wakubwa wamekua na kasumba ya kununua sukari ya TPC na kuificha, ili kuonekane kuna upungufu wa sukari, halafu wanakuja kuitoa kwa bei ya juu zaidi.

Anasema kuna wakala wachache wa TPC, hivyo wanaweza kuungana na kununua sukari yote iliyopo katika maghala yao na kisha wakaificha kwa lengo la kuja kujipatia faida kwa siku za baadae .

"Wakala wa TPC tunawafahamu, hawa wakiungana pamoja, wanaweza kuinunua sukari yote halafu wakaificha ili kuonekane kuna tatizo, halafu wanaanza kuitoa kidogo kidogo," anasema.

Digna Mushi, mkazi wa Sadala ambaye pia ni mfanyabiashara wa maduka ya jumla, anasema wafanyabiashara wanaowauzia sukari ndio wamekuwa wakiwapandishia bei kiholela pasipo taarifa, jambo ambalo si sahihi na inamuumiza mlaji.

"Jiulize kwanini ni sukari ya TPC tu huwa inapanda bei? jibu ni rahisi tu sababu watu walishazoea hivyo hata wakipandishiwa bado watanunua tu," anaeleza

Rai yake ni kwamba, katika kuondoa kadhia hiyo ya upandishaji bei kiholela, kunapaswa kuwapo soko huria, litakalosimamiwa na TPC wenyewe, ili wasambazaji wawe wengi, tofauti na ilivyo kwa sasa.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Kupanda kwa cheo chako si mwisho wa majukumu






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

NIKIWA mdogo nilikuwa na akili za kijasiriamali hivi, kwani nilipenda sana kutunza kila senti niliyopata kutoka kokote, iwe kwa kupewa au hata kuokota.

Na katika akiba, kuna nyakati nilipunguza kidogo kupeleka kanisani kama sadaka na zingine kutumia kwa kitu nilichoona kinanifaa iwe kwa kula au kuvaa.

Siku moja nikaomba ruhusa kwenda mjini, kwani tulikuwa tunaishi kijijini ingawa hakikuwa mbali sana na mjini, baiskeli ilitosha kunipeleka na kurudi.

Hivyo, baada ya ruhusa nikaenda na nikawa nimelenga siku ya mnada, ambao ulifanyika kila Jumapili, nadhani waandaaji mnada ule walilenga siku ya kanisa, kwani kulikuwa na watu wengi.

Nilifika pale mnadani kwa lengo la kununua shati, kwani ni muda sikuwa ama nimenunua au kununuliwa shati na wazazi, licha ya sikukuu kadhaa kupita bila bila.

Hivyo, nikawa nimejipanga kuwashangaza kwa kununua shati zuri ambalo kuanzia familia hata kijiji, ningewashitua kuwa nimelipata wapi.

Nilikuwa mwangalifu sana katika kutafuta shati ambalo litakuwa gumzo katika familia na kijiji chetu. Kwa kweli macho yakaangukia kwenye shati moja hivi la pinki na mapambo.

Vyote hivyo vilinivutia na nikaamini kwamba litatikisa familia na kijiji. Kwa kulitazama tu hivi, nikaamini lingenitosha na sikutaka kupoteza muda, asije mnunuzi mwingine akalichukua nikalikosa.

Mbaya zaidi, hata bei sikubishana na mnunuzi nikijifanya kibopa, nikamtaka tu anifungie kwenye mfuko niwahi kurudi kijijini kabla jua halijazama, nikatambe.

Nilipofika nyumbani, bahati nzuri sikukuta mtu nje, hivyo hakuna aliyeniona nikajitumbukiza ndani na hata bila ya kuoga nikalivaa na kutoka nje, nikakaa kwenye jiwe kusubiri mshangao wa watu.

Mtu mmoja mmoja akatoka nyumbani mwake na kupita akiniona nami nikijifanya simwoni. Wapo walionitazama na kuvunjika mbavu kwa vicheko.

Kwa kweli hakuna aliyeshangaa kama nilivyotarajia na hakuna aliyejitokeza kusema kilichowachekesha. Hivyo, nikabaki kujiuliza kulikoni au nimekosea wapi?

Kweli mshangao ule ulikuwa na maana yake, kwa sababu hatimaye alijitokeza baba ambaye hakusita kuniambia alichokishuhudia na kwa kweli ndicho kilichowachekesha wale wengine.

Kumbe badala ya kununua shati, nilikuwa nimeangukia kwenye blauzi. Ile ilikuwa ni blauzi na kwa rangi yake ndiyo kabisa, baba akaniona mpuuzi kweli kweli, kwa kununua nguo ya kike.

Nilijisikia aibu sana na hivyo nikajisema moyoni na kujilaumu kwa kukurupuka, badala ya kutuliza akili na kuomba ushauri kwa wengine, hivyo sikuwa na la kufanya ila kumzawadia dada yangu. Ilimtosha na aliifurahia akaniombea kwa Mungu.

Kumbe si kila ukitarajiacho kukufurahisha au kukupa faraja ndicho hutokea kwa wakati uliopanga wewe. Haya kumbe hutokea hata katika ngazi za wakubwa nchini.

Juzi kati hapa yakamkuta mzito mmoja wa kiaskari akiwa kwenye mjumuiko wao na ugeni wa mzito zaidi kwenye uongozi wa jamii yake na ndiye aliyemuajiri, akapaza sauti kwa matumaini makubwa kuhusu hoja fulani.

Akaitolea ufafanuzi kwamba kati yao wapo wengi kutokana na promosheni zao, sasa katika nafasi zao kutokana na majukumu waliyo nayo kiaskari leo, ni tofauti na chini walikotoka, sasa hayaendani tena na vyeo hivyo vya zamani ambavyo vinaendana pacha kabisa na jukimu la msingi la uaskari wao - ulinzi.

Hilo lilimshangaza mtoa ajira wao akajiuliza kupanda cheo ndicho kiwazuie namna aliyowapa ajira yao ya kiaskari, ilhali bajeti ya kuwawezesha mishahara yao ni kubwa maradufu.

Tabia hiyo haishangazi, maana hata mwandishi wa habari au wa nafasi fulani akipanda na kuwa mhariri, daima haachi kuandika. Ndiyo sababu hata daktari bingwa wa mifupa, Profesa Philemon Sarungi alipokuwa Waziri wa Afya, hakuacha kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili kutibu wagonjwa. Pigeni mzigo ili kazi iendelee! Alamsiki!

BIASHARA

# Maonyesho Biashara za Wanawake Dar yawafumbua macho wakue zaidi

- Mawaziri wapongeza, watunukiwa nembo
- Wafadhili waahidi hawatochoka kuwasaidia



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima akimkabidhi tuzo mmoja wa wanawake wafanyabiashara waliofanya vizuri wakati wa hafla ya kuwazawadia wanawake wajasiriamali zilizoandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (TWCC). **PICHA: JOSEPH MWANDAPOLE.**

**Na Joseph Mwendapole**

MWANZONI mwa mwezi uliopita, Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (TWCC), kiliandaa maonyesho kwa wafanyabiashara wanawake jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na mamia ya wafanyabiashara kutoka mikoa mbalimbali.

Walionyesha bidhaa mbalimbali za kusindika zikiwamo asali, mboga, matunda, vitenge ambazo ziliwavutia wengi waliowatembelea.

Mgeni rasmi aliyefungua, ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Seleman Jafo, aliyekiri kufurahia namna kinamama walivyoboresha bidhaa zao.

Ni maonyesho yaliyochukua wiki nzima na kufanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam , wananchi wakiwatembelea kuona kazi za mikono za wanawake hao wajasiriamali na yalifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GTZ).

Waziri Jafo anawapongeza wafanyabiashara hao, kwa kupata nembo za ubora kwa bidhaa zao unaowawezesha kuuza kwenye masoko makubwa ndani na nje ya nchi, binafsi akikiri ameona nyingi zina viwango vya kimataifa.

Anasema wanawake hao wameonyesha ujasiri mkubwa kuanzisha vikundi vya uzalishaji bidhaa, hata kuchangia kuongezeka fursa za ajira kwa vijana, wanawake na umma wote nchini.

Waziri Jafo, ambaye kabla ya nafasi yake ya sasa, alikuwa katika Tawala za Mikoa na Serikali ya Mtaa kunakoshughulika moja kwa moja na wananchi, anaisifu Tanzania haikutetereka na ujio wa janga la ugonjwa Covid 19.

Anasema, uimara huo ni zao la wanawake kutoa mchango mkubwa kutengeneza fursa za ajira, kwa kuzalisha bidhaa bora na zinazouzika kimataifa, huku vikundi vyao na vya vijana vikinasa mikopo asilimia 10 kutoka kwenye halmashauri.

"Kuna mabanda nimepita wameniambia wanauza bidhaa ndani na nje ya nchi, hongereni sana kwa hatua hii kubwa mliyopiga, mafanikio haya tuliyofikia ni sababu ya wanawake kuwa mahiri wa kurejesha mikopo kwa wakati," anatamka Waziri Jafo.

Anataja kiu yake sasa ni kuona bidhaa hizo zinasambazwa kwenye maduka mengi makubwa nchini na zingine kusafirishwa nje ya nchi.

**KIONGOZI WA KINAMAMA**

Mwenyekiti wa TWCC, Mercy Sila, anasema chama hicho kinawezesha biashara za wanawake kukua na wengi wameanzia chini, lakini fursa ndizo zimewawezesha, akisema wao ni wasikivu kulipa kodi na baadhi yao wameanzisha kampuni.

> **"Urasimishaji biashara umekuwa rahisi sana na wakala wa usajili wa biashara BRELA anasajili siku moja tu tofauti na ilivyokuwa zamani," anasema Mercy, akimsifu mwanamama mwenzao, mkuu wa nchi.**

"Urasimishaji biashara umekuwa rahisi sana na wakala wa usajili wa biashara BRELA anasajili siku moja tu tofauti na ilivyokuwa zamani," anasema Mercy, akimsifu mwanamama mwenzao, mkuu wa nchi.

Anasema zamani wafanyabiashara wengi walikuwa wakiogopa kwenda katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS), lakini kwa sasa wengi wamefikia viwango na kupewa nembo za ubora na wanarejesha fedha hizo pasipo usumbufu.

Mjasiriamali mshiriki wa maonyesho hayo, Angela Sylivester, anasema amekuwa muhimu kwani wamekutana na wenzao, hata wakabadilishana ujuzi. Angela anawaomba wajasiriamali hao waliopewa mafunzo ya kila mara kuhusu namna bora ya kufungasha bidhaa hizo kuzingatia vipimo sahihi, ili bidhaa zao zikubalike kimataifa.

**OFISA VIPIMO**

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Stela Kahwa, aliyeshiriki maonyesho hayo, anawataka wanawake waendelee kuboresha vifungashio na kuzingatia vipimo sahihi, ili bidhaa zao zikubalike kwenye masoko ya kimataifa.

"Kwenye haya maonyesho ya pili, nimeona tofauti kubwa sana kulinganisha na maonyesho yaliyopita kwa sababu wengi wametumia mafunzo tunayowapa kuboresha ufungashaji na wamejitahidi kuzingatia usahihi wa vipimo ila waendelee kuboresha zaidi," anasema Stela. Anafafanua: "Tumeona makosa madogo madogo kwenye bidhaa zao ambayo yanavumilika na kufundishika na naamini kwa mafunzo tutakayoendelea kuwapa kwenye maonyesho yajayo wataboresha zaidi."

Anasema WMA mbali na kuwapa mafunzo wajasiriamali hao imekuwa ikiwafuatilia kwenye maeneo yao kujua wanavyoendelea na kuwajengea uwezo pale wanapoona wamekwama.

Stela anasema WMA kupitia ofisi zake zilizopo maeneo mbalimbali nchini imekuwa ikiendelea kuwahamasisha wajasiriamali hao wanawake kwa wanaume kuendelea kujitokeza ili kupewa elimu hiyo ambayo manufaa yake ni makubwa.

Anasema wao WMA wamekuwa wakiendelea kuwapa wajasiriamali hao elimu hiyo, kwa lengo la kukidhi matakwa ili kufikia viwango vya ushindani vinavyohitajika.

Ofisa huyo anaahidi kuwa WMA itahakikisha inaendelea kutoa mchango kwa wajasiriamali na maonyesho hayo yanayoandaliwa na TWCC kwa mwaka wa pili sasa.

**YALIVYOHITIMISHWA**

Maonyesho hayo yalihitimishwa kwa wanawake 35 kupewa tuzo ya umahiri kwenye biashara, katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam, mgeni rasmi akiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima.

Anakipongeza Chama cha Wafanyabiashara Wanawake (TWCC) kuandaa tuzo hizo na aliwataka mwakani waongeze idadi ya tuzo hizo hata zifikie 150 ili kuendelea kuwapa moyo wanawake kuendelea kufanya vizuri kwenye biashara.

"Ongezeni idadi ya tuzo hizi hata zifikie 100 na hii itasaidia kuwapa moyo wanawake kwamba wanaweza kufanya mambo makubwa," anasema Waziri Dk. Gwajima

Anasema kuna fursa nyingi za mikopo ya riba nafuu ambayo imekuwa ikitangazwa na serikali na taasisi nyingi za fedha hivyo ni wajibu wa wanawake kuzifuatilia na kuzichangamkia kila zinapotokea.

Mtendaji Mkuu wa (TWCC), Mwajuma Hamza alitangaza vigezo vilivyotumika kuwapata washindi hao na kwamba kulikuwa na majaji watano kutoka taasisi mbalimbali ambao walichuja majina ya wafanyabiashara hao kwenye sekta 16 zilizokuwa zikishindaniwa.

Mwajuma anasema, tuzo hizo zilitolewa baada ya maonyesho hayo ya wiki moja ya wajasiriamali jijini Dar es Salaam, akitaja baadhi ya vigezo husika ni uendelevu wa biashara, mikakati yake na kurasimishwa kuwa na nembo ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), umiliki wake.



## Tume yawezeshwa magari ya mil. 714/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imenunua magari manne ya Sh. milioni 713.9 kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili kurahisisha utendaji kazi.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, aliyasema hayo juzi kwenye uzinduzi wa magari hayo uliofanywa na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Godfrey Pinda, jijini hapo.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha kununuliwa magari hayo ambayo alisema yatasaidia kufanya uchunguzi kwa ajili ya kutafuta haki za binadamu.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutupa fedha hizi. Tunaomba iendelee

kutupa sapoti kwa sababu bado tunahitaji kuongeza magari kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yetu," alisema Jaji Mwaimu.

Pamoja na magari waliyopata katika kutekeleza majukumu ya tume, alisema bado wanahitaji magari kwa ajili ya ufanisi katika utendaji kazi ili kusogeza huduma za kikanda katika mikoa ya Tabora na Njombe.

"Tunaomba serikali iendelee kutupatia fedha za kununua magari zaidi ili kusambaza zaidi huduma kwa wananchi," alisema.

Sambamba na hilo, aliishukuru serikali kwa kutumia vizuri fedha za UVIKO- 19 kwa ajili ya kujenga shule, hospitali za mikoa na wilaya, vituo vya afya ikiwemo kununua vifaa tiba ili kupambana na adui maradhi.

**Pamoja na magari waliyopata katika kutekeleza majukumu ya tume, alisema bado wanahitaji magari kwa ajili ya ufanisi katika utendaji kazi ili kusogeza huduma za kikanda katika mikoa ya Tabora na Njombe.**

# Waliomaliza kidato cha nne watakiwa kubadili tahasusi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema uchaguzi wa wanafunzi kujiunga na kidato cha tano na vyuo vya ufundi, utafanyika baada ya kubadili tahasusi (combination) au kozi walizochagua awali ili wasome wanazozitaka.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Innocent Bashungwa, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema serikali imetoa siku 21 kwa wahitimu wa kidato cha nne ambao wamefaulu katika mtihani wa Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA) mwaka 2021 kufanya mabadiliko ya tahasusi kupitia fomu ya 'selform'.

"Ni matumaini yangu wahitimu watatumia kwa ukamilifu fursa waliyopewa ya kubadilisha tahasusi na kozi kulingana na ufaulu waliopata ili kusoma tahasusi au kozi ambazo wamefaulu vizuri au wana malengo nazo zaidi. Zoezi la wanafunzi kubadilisha machaguo yao litafanyika kuanzia tarehe 30/03/2022 (juzi) hadi Aprili 19," alisema.

Bashungwa alisisitiza kuzingatia muda uliotolewa wa kufanya marekebisho ili ratiba ya kuwachagua na kuwapangia shule na vyuo iendelee vizuri kwa muda uliopangwa.

Alisema pia baadhi ya wanafunzi hawakujaza kwa uhakika tahasusi au kozi zao kutokana na kutokuwa na uhakika wa ufaulu katika masomo yao.

"Hii fursa inatoa mwanya zaidi kwa mwanafunzi kusoma tahasusi au kozi itakayomwandaa kuwa na utaalamu fulani katika maisha yake ya baadaye kwa namna ambayo anatamani yeye mwenyewe au kwa kushauriwa na wazazi au walezi wake sambamba na kadiri ya ufaulu wake kwa mujibu wa matokeo yalivyotoka," alisema. Alisema wanaotaka kubadili machaguo wanatakiwa kuingia kwenye mfumo wa uchaguzi wa wanafunzi (Student Selection MIS) unaopatikana kupitia kiunganishi cha selform.tamisemi.go.tz.

Bashungwa pia alisema serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI imekamilisha utaratibu wa awali wa kuingiza kwenye kanzidata taarifa zilizo kwenye fomu za selform za wanafunzi kama zilivyojazwa na wanafunzi wakiwa shuleni.




Waziri wa Katiba na Sheria, George Simbachawene (katikati), akizindua Ripoti ya Wadau wa Upatikanaji wa Haki nchini Tanzania iliyoandaliwa na Shirika la Legal Services Facility (LSF) chini ya ufadhili wa Taasisi ya Denmark ya Haki za Binadamu, wakati wa uzinduzi wa Kongamano la Msaada wa Kisheria mwaka 2022, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala (wapili kulia) na wadau wa sekta ya msaada wa kisheria. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sheria msaada wa kisheria kupitiwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Katiba na Sheria kwa kushirikiana na Shirika la Legal Services Facility (LSF) wamejadili utekelezaji wa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Hatua hiyo imefanywa katika kongamano la siku mbili la msaada wa kisheria lililofanyika jijini hapa lenye kaulimbiu 'Msaada wa Sheria kwa Jamii Yenye Haki na Jumuishi'.

Akizungumza na waandishi wakati wa tukio la uzinduzi wa kongamano hilo, Waziri wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, alisema kongamano hilo ni sehemu muhimu itakayowaweka pamoja wadau wa sekta ya msaada wa kisheria nchini ili kujadili utekelezaji wa sheria ya msaada wa kisheria na kuangalia namna ya kuboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wake.

"Kabla ya kutungwa na kupitishwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017, wadau wa sekta hii hasa watoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria, walikuwa wakikumbana na changamoto nyingi kubwa ikiwa ni kutokutambuliwa katika taasisi mbalimbali za mifumo ya utoaji haki. Tunatarajia kusikia uzoefu wa wadau hawa na wengine baada ya sheria hii kuanza kutekelezwa," alisema.

Simbachawene alisema kongamano hilo linalenga kupata uzoefu wa utekelezaji sheria za msaada wa kisheria kwa kuangalia maeneo mengine ya nchi jirani kama vile Kenya, Uganda na Malawi huku lengo kuu likiwa ni kupata uzoefu na kujifunza kutoka kwa kila mmoja namna bora ya kukuza sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema kongamano la mwaka huu ni sehemu kubwa ya mafanikio ambayo LSF inajivunia kwa kushirikiana na wadau wengine hasa serikali katika upatikanaji wa haki.

"Tangu mwanzo LSF imekuwa mdau mkuu wa serikali katika kuhakikisha tunaendelea kufanya kazi kwa karibu katika kuwezesha upatikanaji wa haki ikiwamo kuchangia katika kuwezesha sheria ya msaada wa kisheria nchini inapatikana. LSF tumekuwa tukifanya kazi ya kukuza upatikanaji wa haki kupitia uwezeshaji wa kisheria," alisema.Ng'wanakilala alisema kongamano hilo linafanyika sambamba na maonyesho ya wazi kutoka kwa watoa huduma za msaada wa kisheria waliokaa pamoja (one-stop centre) ili kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa watu mbalimbali wanaotembelea maonyesho hayo.

Naye Msajili wa Msaada wa Kisheria, Felistas Mushi, alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano tatizo kubwa imekuwa ada ya usajili wa wasaidizi wa kisheria hata hivyo serikali imeamua kufuta ada hiyo ili kuruhusu wasaidizi wa kisheria kujisajili kwa wingi zaidi.

"Mpaka sasa tuna wasaidizi wa kisheria 757 ambao wamejisajili katika mfumo wa serikali kama watoa huduma za msaada wa kisheria. Vilevile tuna mashirika 202 tu ya wasaidizi wa kisheria yaliyosajiliwa baada ya kukidhi vigezo. Kuanzia mwezi wa pili ada hizo ambazo zilionekana ni kikwazo zimefutwa kabisa," alisema.



# Mil. 600/- zatolewa makundi maalum

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, amekabidhi mkopo wenye thamani ya Sh. milioni 600 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, zilizotolewa na Halmashauri ya Mji wa Tunduma mkoani Songwe kwa ajili ya makundi hayo.

Akikabidhi mikopo wa pikipiki, bajaji na fedha taslimu kwa makundi hayo, Naibu Waziri Silinde alisema kila ifikapo robo ya mwaka Halmashauri ya Mji wa Tunduma imekuwa ikitoa mkopo huo na kwamba lengo ni kuyainua makundi hayo kiuchumi.

"Hatutaki vijana wakae kwenye vijiwe na kubishana kwa ajili ya siasa, ama mpira. Tunataka wawe wanatafuta pesa ili wajikwamue kiuchumi," alisema Silinde.

Aliongeza kuwa zimetolewa pikipiki 90 kwa ajili ya vijana wanaofanya biashara ya usafirishaji abiria maarufu, bodaboda, bajaj 13 pamoja na fedha taslimu na kufanya mikopo ya fedha taslimu na vitendea kazi kufikia kiasi cha Sh. milioni 600.

"Kiu yangu ni kuona kijana anatimiza ndoto za maisha yake kupitia shughuli ya bodaboda, hivyo basi mikopo mnayopewa itawanufaisha ninyi, mtasomesha watoto wenu, mtapata mahitaji muhimu kama chakula na mambo mengine ambayo ninyi mtaona yanafaa," alisema Silinde.

Mkuu wa Wilaya ya Momba, Fakii Lulandala, alisema Halmashauri ya Mji wa Tunduma imekuwa ikitoa mkopo wa mamilioni ya shilingi kila baada ya muda mfupi na hiyo inatokana na uongozi thabiti uliopo.

"Hii mikopo inapatikana kwa sababu mlichagua madiwani wazuri ambao wanaisimamia halmashauri vizuri, lakini hamkukosea kumchagua mbunge wenu makini, David Silinde, amekuwa akihimiza mara kwa mara kuhakikisha mikopo inatolewa kwa walengwa," alisifu.

Alisema Halmashauri ya Mji wa Tunduma imejipanga kuhakikisha inawanufaisha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili waboreshe maisha yao kupitia fedha zake za mapato ya ndani.



Wafanyabiashara wa ndizi katika Mji wa Ushirika wilayani Rungwe mkoani Mbeya, wakimshawishi dereva wa lori kununua bidhaa yao, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Miradi ya maji Mbeya kuwanufaisha maelfu

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amesema zaidi ya wananchi 100,000 katika mkoa huo wanatarajiwa kunufaika na huduma ya maji baada ya Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi na Mazingira Vijijini (RUWASA) kukamilisha miradi mikubwa sita mkoani humo.

Homera alitangaza neema hiyo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema kwa sasa RUWASA wanasimamia miradi mbalimbali ya maji ambapo katika Wilaya ya Chunya wanatekeleza mradi wa Matwiga awamu ya pili ambao unagharimu Sh. bilioni mbili na utawanufaisha wakazi 18,000 baada ya kukamilika ndani ya miezi sita.

Alisema mradi wa maji Matwiga awamu ya kwanza unagharimu Sh. bilioni saba na utahudumia wakazi 56,699 kutoka maeneo ya Mazimbo, Mtanila, Igangwe, Klangali, Luan na Ifuma.

Mkuu wa Mkoa alisema mradi wa maji wa Makongolosi unagharimu Sh. bilioni mbili na utawanufaisha wananchi wapatao 25,000 na utakamilika ndani ya miezi 12 na kuhudumia mji wote wa Makongolosi ulioko wilayani Chunya.

Aliongeza kuwa mradi wa Maji Luduga - Mawindi awamu ya nne na tano unagharimu Sh. bilioni tano na kuhudumia wananchi 40,046 na utakamilika ndani ya miezi 12 na kuvinufaisha vijiji vya Matemela, Kandani, Itipingi, Ipwani na Manienga.

"Mradi wa maji ulioko Mshewe/ Mjele/ Chang'ombe utatumia Sh. bilioni mbili hadi kukamilika kwake kwa kipindi cha miezi 12 na kuhudumia maeneo ya Mshewe, Muvwa, Njelenje, Mapongolo, Mjele na Chang'ombe," alifafanua.

Homera alisema RUWASA Wilaya ya Kyela inatekeleza mradi wa maji wa Ngana ambao unagharimu Sh. bilioni saba na kuwanufaisha wakazi 61,000 na kwamba utakamilika ndani ya miezi 15 na kuvifikia vijiji 24 ikiwamo Ikolo, Lupembe, Bujonde, Nsasa, Ngonga,Mwalisi, Lugombo, Katumbasongwe na Itenya.

Alisema miradi yote hiyo ya maji itagharimu kiasi cha Sh. bilioni 28 na baada ya kukamilika kwake wananchi wataondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya maji safi na salama.

# Watenga miezi minne kutatua mgogoro ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

KAMATI inayoshughulikia mgogoro wa mpaka uliodumu kwa miaka 14 kati ya mfanyabiashara Ismail Mbaga na Shule ya Msingi Mwaka katika Mji wa Tunduma wilayani Momba mkoani Songwe, imeahidi kumaliza tatizo hilo ndani ya miezi minne.

Ahadi hiyo ilitolewa juzi baada ya kamati hiyo iliyo chini ya Mwenyekiti wake, Fank Mponzi, Diwani wa Majengo, kukutana na watu mbalimbali wanaojua mgogoro huo ili watoe maoni yao yatakayosaidia kupata ufumbuzi wake.

Makundi yaliyoitwa na kamati hiyo ni pamoja na viongozi wa dini kupitia mwamvuli wao wa Kamati ya Amani Mkoa wa Songwe, wazee maarufu na wenyeji wa Mji wa Tunduma na Wilaya ya Momba (Chilipamwao).

Akizunguma na waandishi wa habari mara baada ya kikao hicho, mwenyekiti wa kamati hiyo ya usuluhishi kutoka Halmashauri ya Mji Tunduma, Mponzi, alisema wamepokea maoni ya wadau hao ambayo yatawasilishwa kwenye vikao vya baraza la madiwani ili kutafuta ufumbuzi.

"Tumepokea maoni ikiwamo nyaraka mbalimbali na tutapeleka kwenye vikao vya uamuzi na matarajio yetu hadi kufikia Juni mwaka huu, suala hili litakuwa limepatiwa ufumbuzi, alisema.

Shehe Abdilah Alito, aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Amani Mkoa wa Songwe, alisema ana imani kubwa kuhusu utatuzi wa mgogoro huo kwa kuwa walioitwa ni watu sahihi na wenye kujua ukweli wa mpaka sahihi kati ya shule na Ismail.

"Sipendi kutoa tafsiri ya kisheria ila tafsiri ya nini kitatokea baada ya kikao hiki mtaiona kwenye vitendo, ila imani yangu hadi kufikia Juni, mgogoro utakuwa umemalizika kwa kuwa tulioshiriki kutoa maoni yetu hususani wazee, wameeleza ukweli wote," alisema.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma, Abdul Mbwana, Mkuu wa Idara ya Ardhi, alisema kikao hicho kilikwenda vizuri. Alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya halmashauri kuondoa mgogoro huo kwenye vyombo vya sheria.

Mwaka 2008, Halmashauri ya Mji Tunduma wakati huo ikiwa chini ya Wilaya ya Mbozi, ilifungua kesi katika Mahakama ya Ardhi Mbeya ikimshitaki Ismal Mbaga kwa madai ya kuvamia eneo la shule.

Awali, mfanyabiashara huyo aliyedaiwa kuvamia eneo hilo, alionyesha nyaraka mbalimbali zinazoonyesha uhalali wa umiliki wa jengo alilodai kulinunua mwaka 2006 kutoka katika familia ya mtu aliyemtaja kwa jina moja la Dk. Kiendesya.

"Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi iliposikia nimenunua jengo hilo, mwaka 2008 walinifungulia kesi ya uvamizi," alisema.



## Mwinyi awataka viongozi vyama kutoshambuliana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka viongozi wa vyama vya siasa kuzungumzia changamoto zilizoko kwa lengo la kujenga badala ya kushambuliana.

Alitoa angalizo hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari Ikulu Mjini Zanzibar, utaratibu aliouweka kuzungumza nao kila mwisho wa mwezi.

Aliwataka wanasiasa kuweka mbele uzalendo na kuzingatia maslahi mapana ya kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) ambayo lengo lake ni kuwaunganisha wananchi na kuondokana na siasa za chuki na uhasama.

Alisema amani na utulivu ndicho kipaumbele cha kwanza katika serikali anayoiongoza, baada ya kuwepo kwa mpasuko wa kisiasa.

Alizitaja chuki zinazotokana na athari za mivutano ya kisiasa ambapo ilifika wakati watu walipoteza maisha kutokana na vurugu na wengine kupeana talaka kutokana na tofauti za kisiasa, na kwamba wapo waliokimbia nchi na Zanzibar kutoa wakambizi. Alisema njia pekee zinapotokea changamoto za aina hiyo ni viongozi kukaa pamoja na kuzipatia ufumbuzi na kamwe kutokubali kurudi walikotoka.

"Ndugu wananchi dhamira yangu ya kuwaunganisha wananchi ipo pale pale...wanasiasa zinapotokea changamoto za aina hiyo tukae chini ya kuzizungumza kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi na huu sio wakati wa kujibishana," alisema Rais Mwinyi.

Alisisitiza kwamba hakuna uchumi na uwekezaji bila ya amani, na kwamba suala hilo ndicho kipaumbele kikubwa cha Serikali ya Zanzibar.

"Nimeamua kwanza kulitolea ufafanuzi suala hili, sina sababu ya kujibu kwani hakuna maslahi ya uchumi na uwekezaji bila ya amani," alisisitiza.

Dk. Mwinyi alisema mivutano ya kisiasa na uchumi katika baadhi ya mataifa ya Ulaya ikiwamo Ukraine na Russia kwa kiasi kikubwa yamesababisha kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali yakiwamo mafuta ya kupikia na unga wa ngano.

# Wawakilishi wataka viwango ujenzi wa shule kwa fedha za UVIKO-19

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAMATI ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi imeitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufuatilia kwa karibu miradi ya ujenzi wa shule inayotokana na fedha za ahuweni ya ugonjwa wa UVIKO-19 na kuona zinajengwa kwa kuzingatia ubora wa viwango.

Maelekezo hayo yalitolewa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mohamed Ahmada, alipotembelea miradi ya sekta ya elimu inayotokana na fedha za ahuweni ugonjwa huo kisiwani Pemba.

Alisema serikali imetenga jumla ya Sh. bilioni 35 kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya elimu ya shule za ghorofa na kuzikarabati nyingine nane, hatua ambayo itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi.

Ahmada alisema uzoefu unaonyesha baadhi ya miradi ya ujenzi wa shule zilizojengwa miaka ya nyuma hazikuwa na viwango, na matokeo yake baada ya miaka miwili zimeonyesha nyufa na ubovu.

"Watendaji wa Wizara ya Elimu tunawaomba mfuatilie kwa karibu sana miradi ya ujenzi wa shule za sekondari Pemba zikiwamo za ghorofa pamoja na ukarabati wa shule kongwe," alisema.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, alisema ujenzi wa shule za ghorofa katika kisiwa cha Pemba unaendelea vizuri pamoja na ukarabati wa shule kongwe ikiwamo ya Fidel Castro.

Alisema ukaguzi wa miradi ya shule hizo unafuatiliwa kwa karibu sana na makandarasi walioko katika wizara kuona ubora wa majengo unazingatiwa.

"Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Kamati ya Ustawi wa Jamii, Wizara imejipanga kikamilifu kuona miradi inayotekelezwa katika sekta ya elimu inazingatia viwango vya ubora na usanifu wa majengo," amesema.

Alisema ujenzi wa shule tatu za ghorofa katika kisiwa cha Pemba pamoja na ukarabati wa shule kongwe tatu kwa kiasi kikubwa utasaidia kuimarisha sekta ya elimu na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

Alikiri kuwapo kwa msongamano mkubwa wa wanafunzi darasani ambapo wakati mwingine hulazimika wanafunzi kuingia katika vipindi tofauti, hivyo kuzorotesha maendeleo ya elimu.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Atupele Mwakibete (wapili kulia), akipokea kitabu cha huduma kwa mteja na mfumo wa malalamiko kwa wateja uliobuniwa na watumishi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TCAA, Hamza Johari, baada ya kuzindua Baraza la Wafanyakazi wa mamlaka hiyo, jijini Tanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kaimu Jaji Mkuu ataka Kiswahili kortini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAIMU Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Shaaban, amesema wakati umefika kwa majaji na mahakimu kutumia lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa kesi na utoaji wa hukumu.

Shaaban alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na wadau wa mfumo wa haki jinai Tunguu Wilaya ya Kati ambapo suala la matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuendesha kesi mahakamani lilijadiliwa na kuchukua nafasi kubwa.

Alisema Mahakama Kuu ya Zanzibar ipo katika maboresho makubwa ya uendeshaji wa shughuli zake ambao umejikita zaidi katika mfumo wa sayansi na teknolojia.

Alisema mfumo huo utaziunganisha mahakama zote na mawasiliano ya teknolojia ambapo majaji na mahakimu watakuwa wakiwasiliana katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwamo pia mwenendo wa kesi mahakamani.

"Nataka niwaambie majaji na mahakimu pamoja na waendeshaji mashtaka na Jeshi la Polisi kwamba tupo katika hatua za mwisho za maboresho ya uendeshaji wa shughuli zetu ambao umejikita katika sayansi na teknolojia na mawasiliano," amesema.

Aliwataka majaji na mahakimu kuhakikisha kwamba wanaendesha kesi pamoja na kutoa hukumu kwa lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo inayotumiwa na wananchi wengi.

Alisema kwa nyakati tofauti viongozi wakuu wa nchi wamesisitiza umuhimu wa mahakama kuendesha kesi na kutoa hukumu zitakazoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ili waweze kujua mwenendo wa kesi na hatua za kukata rufani.

"Mahakama Kuu tumeanza kutekeleza maagizo muhimu ya viongozi wakuu wa nchi ya kututaka kutumia lugha ya Kiswahili katika uendeshaji na utoaji wa hukumu zetu kwa wananchi," alisema.

Baadhi ya viongozi watendaji wa taasisi za sheria na mwenendo wa jinai wametaka kuongezwa kwa kasi ya uchunguzi wa kesi mbalimbali ili haki itendeke katika utoaji wa hukumu.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Salma Ali Hassan, alisema kuchelewa kukamilika kwa uchunguzi wa baadhi ya kesi zikiwamo za jinai ni moja ya changamoto kubwa ambayo wananchi wamekuwa wakivitupia lawama vyombo vya sheria.

"Vyombo vinavyosimamia mwenendo wa kesi za jinai wakati umefika kuona kesi hizo zinasikilizwa kwa haraka na kutolewa hukumu yake kwa wakati,"alisema.

Jaji wa Mahakama Kuu, George Kadhi, alisema wamejipanga kuhakikisha mashauri mbalimbali yanayofikishwa mbele ya mahakama yanasikilizwa na wakati na kutolewa hukumu yake, hatua ambayo itasaidia jamii kujenga imani zaidi mbele ya vyombo vikuu vya kutoa haki na maamuzi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMMANUEL YONA SAMO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0534/0121** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ST.ANTHONY'S** mwaka 2012, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/130269/2022**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ABRAHAM STANSLAUS MAGUNIRA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0632/0058** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya BONDENI mwaka 2005,na cheti cha kurisiti chenye index namba **P0632/0197** kilichotolewa BONDENI secondary mwaka 2006, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/113112/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**THELESIA DEUSI LINTU** antangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA FUN CARGO** yenye NAMBA ZA USAJILI **T711 BSB**, CHASSIS NAMBA **NCP210005084,** INJINI NAMBA **1NZ1052795** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

TAARIFA POLISI:
**ARU/ARU/RB/129453/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ............TANGA**

**Kituo cha..... MJINI TANGA.... Mkoa... TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi............74............2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: HAMISI SALIMU MANDARO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA: SHAMRA SALIMU MWANDARO**

### TANGAZO

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07/04/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo 30/03/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF BUKOBA**
**AT BUKOBA**

**LAND CASE APPEAL.76/2021**

**Arising from land Application case no 84/2013 no DLHT of Bukoba**

**DOMINIC KATEMA....................................APPLICANT**

**VERSUS**

**PASKAZIA THADEO........................................1st RESPONDENT**
**GODWIN MUTEKANGA....................................2ND RESPONDENT**
**ANAMARIA DEOGRATIAS................................3RD RESPONDENT**
**PHILIMON SIMON...........................................4RD RESPONDENT**
**SADICK ATHUMAN..........................................5TH RESPONDENT**

**TO.PHILIMON SIMON**
**SADICK ATHUMAN**

### RE:NOTICE FOR DATE OF HEARING

Whereas the above mentioned Appellants has lodged a case registered as Misc Land case application no 76/2021 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.Take notice that the above case has been scheduled for hearing on 25thday of April,2022 at 08:30 am before Hon Mwipopo J.You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that day and time for the said mention the case will proceed in your absence Given under my hand and seal of the court this 17TH day of March,2021

J.MASSESA
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

## BANI INVESTMENT LIMITED
DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS

### NYONGEZA YA TANGAZO LA MNADA

Minada yote iliyotangazwa na **BANI INVESTMENT LTD Tarehe 31.3.2022** itafanyika kama ilivyopangwa kuanzia **4:00 (saa nne kamili)** asubuhi nakuendelea.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**
BANI INVESTMENT LTD, S.L.P 71340 Dar es Salaam Lida Building, ghorofa ya 3 chumba No. 0313 Nkrumah Street. Tel. 0713 224 578, 0754 688059, 0713 295747

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Zelensky: Tunajiandaa na mashambulizi mapya



Wanajeshi wa Russia wakiwa kwenye moja ya paredi kitaiifa. Jana, Rais Vladimir Putin amesaini amri ya kuagiza wanajeshi wapya 134,500, Wizara ya Ulinzi imesema wito huo hauhusiani na vita vya Ukraine. **PICHA: MAKTABA**

**Kyiv,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amesema nchi yake inajiandaa kwa mashambulizi mapya kutoka Russia, eneo la Mashariki, mjini Donbas, ikiwa ni takribani wiki ya sita tangu mashambulizi kati ya nchi hizo yaanze.

"Kuna mkusanyiko wa wanajeshi wa Russia kwa ajili ya mashambulizi mapya mjini Donbas. Na wanajiandaa kwa hili," amesema katika taarifa, jana.

Ameelezea wasiwasi wake juu ya taarifa ya Russia wakati wa mashauriano ya kupunguza shughuli za kijeshi karibu na mji mkuu wa Kyiv na mji wa Chernihiv.

"Hatumwamini mtu yeyote, hatuamini maneno mazuri kutoka kinywani mwa mtu yeyote," Zelensky amesema.

Ameongeza kwamba hakuna sababu ya kuamini matangazo ya Russia, ikisema itasitisha operesheni ya kijeshi karibu na miji hiyo, ikizingatiwa vikosi vya Russia, vinaendelea na mashambulizi ya anga mjini Kyiv na Chernihiv, siku moja baada ya kutoa ahadi ya kusitisha mapigano.

Mashambulizi mabaya pia yameripotiwa mji wa Irpin, pamoja na mashambulizi makali katika mkoa wa Donbas.

Zelensky pia amesisitiza dhamira ya Ukraine ya kulinda eneo lao, akisema "Hatutaacha chochote. Na tutapigania kila mita ya ardhi yetu, kwa kila mtu."

Hata hivyo, Kremlin imeelezea madai yaliyotolewa na Marekani kwamba Rais wa Rais Putin, anapotoshwa na washauri wake kuhusu Ukraine.

Katika kikao chake na wanahabari cha kila siku, Msemaji wa Kremlin, Dmitry Peskov amewaambia waandishi wa habari kwenye makao makuu ya Russia, mjini Moscow, kwamba si Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, wala Pentagon, yenye taarifa za kweli kuhusu kile kinachotokea.

"Hawaelewi kinachoendelea katika Kremlin," amesema.

"Hawaelewi Rais Putin, hawaelewi jinsi maamuzi yanachukuliwa na hawaelewi mtindo wa kazi yetu."

Aidha, Ukraine imeendelea, kutuma mabasi kwenda mji wa Mariupol kutoa msaada, kuwahamisha raia baada ya Russia kutangaza kusitisha mapigano kwa mji wa bandari uliozingirwa, Kusini Mashariki mwa nchi hiyo.

Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine, Iryna Vereshchuk, amesema katika ujumbe wake katika video kuwa mabasi 45 yametumwa mjini Mariupol, akisema wanafanya kila liwezekanalo kuhakikisha mabasi hayo yanafika na kuwachukuwa watu ambao bado hawajaondoka.

Msafara wa mabasi ulitarajiwa kubeba watu jana kutoka Mariupol kuwapeleka Zaporizhzhia, umbali wa karibu kilomita 300, kupitia mji unaodhibitiwa na Russia wa Berdyansk.

Juhudi kadhaa za kuwaondoa raia zimekwama kutokana na kushindwa kuweka njia salama za kutokea, katikati mwa mapigano.

Mji wa Mariupol, ulio kwenye bahari ya Azov, umezingiriwa na vikosi vya Urusi tangu mwanzoni mwa mwezi Machi.

Uturuki bado inasimamia mahala pake kwa kushinikiza kuwaleta pamoja mawaziri wa mambo ya nje wa Ukraine na Russia, kwa ajili ya mazungumzo.

Waziri Mkuu wa Norway, Jonas Gahr Stoere amefanya mazungumzo ya kina na Rais Putin kwa njia ya simu: Nimempa wito rais kusitisha vita Ukraine, na kuondoa majeshi," amesema Stoere.

Norway, ni mwanachama wa NATO ambaye inayopakana na Russia kwenye mpaka wa Arctic.

**WAKIMBIZI SASA MIL. 4**

Umoja wa Mataifa (UN), umesema idadi ya wakimbizi kutoka Ukraine kwenda nchi jirani, imeongezeka na kufikia milioni nne kati ya hao milioni 2.3 wakielekea nchini Poland.

Tangu mashambulizi ya Russia dhidi ya Ukraine yaanze Februari 24, mwaka huu, wimbi kubwa la raia kuondoka Ukraine inaongezeka wengi wao wakiwa wanawake na watoto.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) limesema kwamba hata ndani ya Ukraine watu milioni 6.5 wameyahama makazi yao.

**POLAND YASITISHA UAGIZAJI MAFUTA**

Poland, imetangaza hatua za kusitisha uagizaji wa mafuta ya Russia, ifikapo mwishoni mwa mwaka huu, wakati Ujerumani ikitoa onyo kuhusu bidhaa za gesi asilia na kuwataka watumiaji kuhifadhi nishati.

Hiyo ni ishara ya kuongezeka kwa mvutano wa kiuchumi barani Ulaya kuhusiana na vita vya Russia nchini Ukraine.

Waziri Mkuu wa Poland, Mateusz Morawiecki, amesema nchi yake inazindua mpango mkubwa miongoni mwa mataifa ya Ulaya wa kuondokana na vyanzo vya nishati ya Russia.

Poland imesema, inapiga marufuku uagizaji wa makaa ya mawe kutoka Russia.

Morawiecki, ameyataka mataifa mengine ya Ulaya kutoagiza mafuta ya Russia, akisema kuwa mapato ya mafuta na gesi yanaisaidia Russia kuendesha vita.

Nchini Ujerumani, Waziri wa Uchumi Robert Habeck, ameonya kuhusu wasiwasi kuwa Russia huenda ikasitisha usambazaji wa gesi asilia, kama haitolipwa katika sarafu ya Kirusi ya 'Ruble'.

Mataifa ya Magharibi yamepinga sharti la Russia la malipo ya fedha ya nchi hiyo, kwa hoja kuwa itakiuka vikwazo vilivyowekwa dhidi ya Moscow.

**UCHAGUZI KENYA 2022:**

**Zaidi ya Wakenya milioni 24 wajisajili vyama kisiasa**

KUELEKEA uchaguzi mkuu Kenya, idadi ya Wakenya kujisajili kwenye vyama tofauti vya kisiasa imeongezeka, karibu mara mbili ikiashiria hamasa kisiasa kupanda hususani maandalizi ya uchaguzi wa Agosti 9, mwaka huu.

Idadi ya Wakenya kufikia sasa imefikia milioni 24 kutoka wanachama milioni 16 wa vyama vya kisiasa waliotangazwa mwaka wa 2013.

Kati ya hao, milioni 15.4 ni wanaume huku 8.6 wakiwa wanawake.

Zaidi ya vyama 82 vya kisiasa pia vimewasilisha usajili wao wa vyama, huku Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (ORPP), imeanza mchakato wa uhakiki ambao utachukua siku saba.

"Ofisi itaanza uthibitishaji ndani ya siku saba na kuwasilisha kwa msajili aliyeidhinishwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC). Pia tutaweka orodha ya wanaowania dhidi ya rejista ya uanachama na hatimaye kutoa rejista iliyoidhinishwa ya uanachama kwa vyama vya siasa." Msajili wa Vyama vya Siasa, Anne Nderitu, amesema.

Mchakato huo pia utahusisha mambo mengine kama uthibitisho mtu kuwa raia wa Kenya, mtu mzima na hajihusishi na zaidi ya chama kimoja cha kisiasa.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

HABARI MICHEZO

# TEMBO WARRIORS WAIANGUKIA SERIKALI ADA KOMBE LA DUNIA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Chama cha Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu nchini (TAFF), umeiomba serikali kuwasaidia kulipa ada kiasi cha dola za Marekani 5,000 sawa na Sh. milioni 11.5 za Tanzania ili kupata kibali cha timu ya Taifa ya Tanzania 'Tembo Warriors', kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa TAFF, Peter Sarungi, alisema wamepokea taarifa kutoka Shirikisho la Soka la Watu wenye Ulemavu Duniani (WAFF), wakitakiwa kulipa ada ya ushiriki mapema na watakaoshindwa kulipa wataondolewa katika mashindano hayo.

Alisema ameikumbusha serikali kwamba wanatakiwa kutekeleza suala hilo mapema ili Tanzania isiwe miongoni mwa timu ambazo zitapokwa nafasi hiyo ya kwenda kushiriki Kombe la Dunia.

"Tunatakiwa kulipa ada ya dola 5,000 kila taifa ambalo limefuzu kushiriki mashindano hayo na usipolipa unaondolewa na nafasi kupewa nchi nyingine, kwa ukanda wetu wa Afrika Mashariki na Kati, Kenya wamekuwa wakihitaji nafasi hiyo," alisema Sarungi.

Alisema hata kama Taifa limefanikiwa kufuzu kucheza mashindano hayo kama ada hiyo ya ushiriki haikulipwa asipolipa huondolewa na nafasi kupewa nchi ambayo itakuwa tayari kulipa.

Tanzania kupitia timu ya watu wenye ulemavu, wamefanikiwa kufuzu mashindano hayo baada ya kufanya vizuri katika michuano ya CANAF, hivyo kukata tiketi ya kwenda kushiriki fainali hizo zitakazofanyika nchini Uturuki, Oktoba mwaka huu.

Tembo Warriors kwa sasa ipo kambini jijini Dar es Salaam na Juni, 2022 inatarajia kwenda mikoa ya baridi ukiwamo Arusha au Njombe kwa ajili ya kambi ya awamu ya pili kabla ya kwenda nchini Uturuki.

MAZOEZI



Wachezaji wa timu ya watu wenye walemavu, wakifanya mazoezi ya viungo katika viwanja vya Kituo cha Jakaya Kikwete (JMK), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Namungo imara kuivaa KMC FC

**Na Saada Akida**

LICHA ya kujiandaa vizuri kwa kucheza mechi za kirafiki kambini nchini Zambia, Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio', wanatarajia kupata ushindani mkubwa Jumapili wiki hii katika mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya wenyeji wao, KMC FC.

Namungo FC watakuwa ugenini kuwakabili KMC FC Katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Julio alisema kambi waliyoweka nchini Zambia na mechi za kirafiki walizocheza zimewasaidia katika maandalizi ya mchezo huo ambao anaamini utakuwa na ushindani mkubwa kutokana na ubora wa wapinzani wao ukichagizwa na kuwa na mwalimu mzuri.

"Mechi ni ngumu kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji matokeo, tumejiandaa vizuri kambi yetu ya Zambia imetunufaisha na mambo mengi ikiwamo mechi za kirafiki kujua mapungufu ya kikosi chetu pia," alisema Julio.

Alisema kikosi chao kipo vizuri na wako tayari kwa mchezo huo kuhakikisha wanapata matokeo chanya ili kujiimarisha katika nafasi za juu katika msimamo wa ligi hiyo ambayo kinara ni Yanga ikiwa na pointi 48.

Namungo FC iko nafasi ya nne ikiwa na pointi 25 na kama ikifanikiwa kushinda mechi hiyo itafikisha alama 28 sawa na Azam FC inayoshika nafasi ya tatu nyuma ya Simba yenye pointi 37 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kwa upande wa KMC ipo nafasi ya saba ikiwa na alama 22 baada ya kushuka dimbani mara 18 kama ilivyo kwa timu zote 16 za ligi hiyo.

# Plan International kuinua Soka la Wanawake

**Na Vitus Audax, MWANZA**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Plan International, jijini Mwanza, limeahidi kuzidi kuinua mchezo wa mpira wa miguu kwa wasichana kupitia mashindano mbalimbali shuleni.

Akizungumza baada ya ugawaji wa zawadi kwa washindi wa michuano ya mpira wa miguu kwa shule za msingi zilizoko wilaya za Ilemela na Nyamagana, Mratibu wa Plan International, Benadetha Mazura, alisema dhumuni lao ni kuinua soka la wasichana mkoani humo kupitia wanafunzi waliopo shuleni.

"Lengo letu ni kuhakikisha mtoto wa kike anashiriki michezo yote hususan mpira wa miguu, na kupitia hilo tumeanza na haya mashindano yaliyoshirikisha wanafunzi wa shule za msingi kutoka Wilaya za Nyamagana na Ilemela hapa mkoani Mwanza yaliyoanza tangu Machi Mosi na kuhitimishwa Machi 30," alisema

Katika mashindano hayo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza na timu ya Shule ya Msingi, Chasubi kutoka Ilemela iliibuka vinara katika mchezo huo kwa ushindi wa mabao 4- 2 dhidi ya Shule ya Msingi Luchelele ya Wilaya ya Nyamagana.

Farjala Msagati, Mwalimu wa michezo wa Chasubi, akielezea siri ya ushindi huo alisema: "Tumekuwa tukishirikiana zaidi walimu wote katika kuhakikisha tunawanoa hawa vijana wetu na ndio imekuwa siri ya ushindi huu, kila mwalimu alikuwa akijitahidi kuchukua kundi lake na kulipa mafunzo."

Kwa upande wa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Luchelele na Kocha wa timu hiyo, Kilian Yameseo, alitoa shukran kwa Shirika la Plan International kwa udhamini wao katika michezo hiyo na kuahidi kufanya vizuri katika michuano itakayojitokeza tena ikiwamo Umitashumta.

"Kikubwa zaidi nawashukuru Plan international kwa kuandaa michuano hii pia kwa udhamini wa jezi pamoja na mipira. Tulitaraji kuwa washindi wa michuano hii, lakini timu pinzani wamedhibiti mbinu zetu na kutufunga, tutajitahidi zaidi katika mashindano yajayo likiwamo ya Umitashumta," alisema,

Shirika la Plan International, Machi Mosi lilianzisha michuano hii ambayo ilifikia kilele juzi, Jumatano, shule 36 zikishiriki michuano hiyo kutoka wilaya za Nyamagana na Ilemela, huku mshindi wa Kwanza akiibuka na zawadi ya kombe la ubingwa, mpira pamoja na boksi la daftari. Mshindi wa pili akijinyakulia mpira pamoja na boksi la daftari vivyohivyo kwa mshindi wa watatu wakati washiriki wengine waliofika 10-bora wakijipatia zawadi ya boksi la daftari kwa kila timu.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### ABRAHAM ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United ipo tayari kumnunua mshambuliaji wa England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 24, ambaye amefunga mabao 23 katika klabu ya Roma ya Italia msimu huu. ***(Corriere dello Sport)***

### MARTIAL KUMBADILISHA KANE

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26, anaweza kutumiwa na Manchester United kama suluhu katika mpango wa kumsaini nahodha wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28 kutoka Tottenham Hotspur. ***(ESPN)***

### PHILLIPS KUBAKI LEEDS

KIUNGO wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 26, ameiambia Leeds United kuwa anataka kusaini mkataba mpya msimu huu, ambao unaweza kuwakatisha tamaa Manchester United, Liverpool, Newcastle, West Ham na Aston Villa. ***(Mirror)***

### EVERTON KUUZA NYOTA

KLABU ya Everton italazimika kumuuza mmoja wa washambuliaji wake nyota, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 25 au mchezaji wa kimataifa wa Brazil Richarlison miaka 24, kipindi cha msimu wa majira ya joto baada ya kupata hasara ya pauni milioni 121 msimu uliopita.***(Sun)***

### NUNEZ AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inatamani kumnunua mshambuliaji wa Benfica mwenye thamani ya pauni milioni 60, Darwin Nunez, lakini matumaini yao ya kumpata mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay yanategemea kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Telegraph)***

### HICKEY KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United ipo tayari kumnunua beki wa Bologna na Scotland, Aaron Hickey mwenye umri wa miaka 19, ambaye anaweza kuruhusiwa kuondoka klabu hiyo ya Italia kwa kati ya pauni milioni 15 hadi 20. ***(Fabrizio Romano)***

### BERGWIJN KUMALIZA MUDA

NYOTA, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24, amedokeza kwamba yuko tayari kumaliza muda wake Tottenham Hotspur. ***(Mail)***

### SCHICK HAONDOKI LEVERKUSEN

MSHAMBULIAJI wa Jamhuri ya Czech mwenye umri wa miaka 26, Patrik Schick, ambaye amehusishwa na uhamisho wa kwenda Arsenal au Barcelona, hataondoka Bayer Leverkusen, amesema Afisa Mkuu mtendaji wa klabu hiyo. ***(Goal)***


### KANTE KAIKATAA PSG

KIUNGO wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31, alipuuza ombi la la Januari kutoka kwa Paris St-Germain la kujiunga nao msimu huu wa joto. ***(Le Parisien)***

### MILAN WAMTAKA ANSENSIO

KLABU ya AC Milan inatafakari uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Real Madrid, Marco Asensio baada ya kurudi nyuma kutokana na masharti ya mshahara wa kiungo huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 26. ***(Tuttosport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DYBALA ACHAGUA KWENDA KUITUMIKIA ATLETICO MADRID

●●●Kitendo cha klabu hiyo kumkosa Martinez kunatoa wigo wa kuweza kumpata nyota huyo wa Juve ambaye...

**TURIN, Italia**

MSHAMBULIAJI nyota wa Juventus, Paulo Dybala ameichagua Atletico Madrid kama klabu ambayo anahitaji kwenda kucheza baada ya kuondoka kwenye viunga vya Turin mwishoni mwa msimu kama mchezaji huru.

Mazungumzo kati ya Juventus na Dybala yameshindakana kutokana na kushindwana kwenye masuala ya makubaliano ya mshahara, na anajiandaa kuachia kitambaa cha unahodha na jezi namba 10 pindi tu msimu utakapomalizika.

Nafasi ya Dybala imekuwa shakani tangu kusajiliwa kwa Dusan Vlahovic, ambaye ametokea klabu ya Fiorentina wakati wa dirisha la Januari.

Dybala bado yuko kwenye kiwango kizuri msimu huu huku akifanikiwa kufunga mabao 13 na kutoa asisti sita katika michezo 29 aliyocheza.

Atletico Madrid wapo kwenye rada ya kuhitaji saini ya Laurato Martinez, lakini hawako tayari kulipa euro milioni 70 kama ada ya usajili ya kumuondoa kwenye dimba la San Siro, wakati mwaka 2018 alishafanyiwa mpaka vipimo vya afya pia aliondoka kwenye kambi ya timu ya taifa ili kujiunga na Atletico, lakini ilishindikana.

Atletico Madrid kumkosa Martinez kunatoa wigo wa kuweza kumpata Dybala pasipo gharama kubwa kwa Diego Simeone ambaye amepanga kuingia sokoni ili kuweza kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.


LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,089

MECHI KALI
POLISI TANZANIA
VERSUS
RUVU SHOOTING
1 | 2.10
X | 2.82
2 | 3.70

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
GBT:0249

# KUYT: TEN HAG SAHIHI MAN UNITED



**MANCHESTER, England**

MCHEZAJI wa zamani wa Liverpool, Dirk Kuyt, anaamini kuwa Manchester United watakuwa wameokota dodo kwenye mpera ikiwa tu watampa kazi Erik Ten Hag kama mrithi wa mikoba ya kocha wa muda, Ralf Rangnick.

Man United kwa sasa ipo kwenye mchakato wa kutafuta kocha atakayerithi mikoba ya Rangnick ambaye mwisho mwa msimu anaenda kuwa mkurugenzi wa ufundi.

Kuyt akizungumza na waandishi wa habari, alisema, "Ten Hag ni kocha bora, mwenye uzoefu, tayari amejifunza vya kutosha, amefanya kazi kwenye klabu ya Bayern Munich kama kocha msaidizi, baadaye Utrech na sasa Ajax.

"Ni kocha bora ambaye amejiimarisha sana, ndani na nje ya uwanja. Najua kuna watu wanawasiwasi na uzungumzaji wake wa lugha ya Kingereza, jinsi anavyozungumza mbele ya kamera, lakini unaona jinsi anavyoimarika siku hadi siku kama kocha na nadhani anaweza kuwa kocha bora kwenye timu yoyote kubwa Ulaya.

"Mbinu zake, jinsi anavyofikiria kuhusu mpira, inavutia, na itakuwa vizuri kama atapata nafasi ya kufundisha timu kubwa."

Ten Hag ni moja ya chaguo linalopigiwa upatu kuweza kuchukua mikoba ya kuinoa Man Utd akiwamo pamoja na Mauricio Pochettino, Luis Enrique na Julen Lopetegui.

# Chelsea kuendelea kuvaa nembo ya 3

**LONDON, England**


KLABU ya Chelsea itaendelea kuvaa nembo ya 3 kwenye jezi zao licha ya kampuni hiyo kusitisha udhamini wa pauni milioni 40 kwa mwaka kutokana na klabu hiyo kuwekewa vikwazo na Kampuni ya Nike kutoruhusiwa kuwatengenezea vifaa vipya.

Kampuni hiyo ya mawasiliano ilisitisha udhamini wake wenye thamani ya pauni milioni 40, siku ambayo mmiliki wa klabu hiyo aliwekewa vikwazo na kuitaka klabu ya Chelsea kuondoa nembo yao kwenye jezi zao haraka iwezekanavyo.

Lakini ombi lao halijaweza kufanikiwa, chini ya kibali maalumu ambacho klabu ya Chelsea imepewa kwa ajili ya uendeshaji, lakini mtengenezaji wa jezi hataruhusiwa kutengenezea jezi mpya.

Chelsea wametumia jezi zenye nembo ya 3 kwenye michezo minne tangu Abramovich awekewe vikwazo, kwenye kipindi hichi cha mapumziko ya mechi za kimataifa, wamejaribu kutatua hili tatizo lakini imeshindikana, walikuwa na mpango wa kuzipaka rangi sehemu yenye nembo ya 3 lakini wamekataliwa.

Mdhamini mwingine aliyejitoa ni Hyundai ambaye nembo yake ilikuwa mikononi lakini hawakuomba nembo yao itolewe.



## HABARI MICHEZO


9,062,840

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 02/04/22 | 17:00 | Leeds vs Southampton | 2.36 | 3.53 | 2.83 |
| 02. 02/04/22 | 17:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 2.84 | 3.09 | 2.54 |
| 03. 02/04/22 | 19:30 | Borussia Dortmund vs RB Leipzig | 2.38 | 3.59 | 2.69 |
| 04. 03/04/22 | 14:00 | Rangers vs Celtic | 2.36 | 3.28 | 2.88 |
| 05. 03/04/22 | 15:30 | Fortuna Sittard vs Heracles Almelo | 2.58 | 3.28 | 2.58 |
| 06. 03/04/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.56 | 2.96 | 2.96 |
| 07. 03/04/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Nantes | 2.55 | 3.05 | 2.90 |
| 08. 03/04/22 | 16:00 | Atalanta vs Napoli | 2.42 | 3.20 | 2.90 |
| 09. 03/04/22 | 16:30 | Augsburg vs VfL Wolfsburg | 2.86 | 3.26 | 2.45 |
| 10. 03/04/22 | 19:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.59 | 3.03 | 2.79 |
| 11. 03/04/22 | 19:30 | Granada vs Rayo Vallecano | 2.68 | 3.13 | 2.73 |
| 12. 03/04/22 | 20:00 | Moreirense vs Vitoria Guimaraes | 2.80 | 3.20 | 2.47 |
| 13. 03/04/22 | 21:45 | Juventus vs Inter | 2.70 | 3.25 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 01/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 3972 | Perth Glory Youth vs Floreat Athena | 2.07 | 3.65 | 2.92 |
| 15:00 | 2483 | NK Dubrava vs Cibalia Vinkovci | 1.77 | 3.51 | 3.99 |
| 15:00 | 5488 | Aizawl FC vs Gokulam Kerala FC | 3.31 | 3.36 | 2.00 |
| 16:00 | 5158 | Polisi Tanzania vs Ruvu Shooting | 2.10 | 2.82 | 3.70 |
| 18:00 | 3160 | Viktoria Otrokovice vs Kromeriz | 5.07 | 4.78 | 1.44 |
| 19:00 | 1367 | Opava vs Jihlava | 1.62 | 3.84 | 4.47 |
| 19:00 | 2945 | Rubin Kazan vs FK Khimki | 2.53 | 3.08 | 2.78 |
| 19:00 | 5530 | Zbrojovka Brno vs Pribram | 1.43 | 3.99 | 6.62 |
| 19:00 | 5653 | Sandecja vs Korona Kielce | 2.53 | 3.07 | 2.63 |
| 19:00 | 5797 | Stal Mielec vs Cracovia | 2.96 | 3.06 | 2.29 |
| 19:30 | 1556 | Dynamo Dresden vs Schalke 04 | 3.72 | 3.47 | 1.91 |
| 19:30 | 1737 | Ingolstadt vs Erzgebirge Aue | 2.35 | 3.27 | 2.87 |
| 20:00 | 1068 | Leixoes vs Penafiel | 2.06 | 3.20 | 3.49 |
| 20:00 | 2121 | HIK Hellerup vs AB Gladsaxe | 2.36 | 3.37 | 2.63 |
| 20:00 | 4073 | Tuzlaspor vs Umraniyespor | 3.30 | 3.16 | 2.08 |
| 20:30 | 4742 | Yverdon vs Sport FC-FC Vaduz | 2.19 | 3.31 | 2.92 |
| 20:30 | 4846 | FC Schaffhausen vs Neuchatel Xamax | 1.85 | 3.54 | 3.59 |
| 21:00 | 1199 | NAC Breda vs Jong Ajax | 2.25 | 3.76 | 2.67 |
| 21:00 | 1250 | FC Volendam vs FC Oss | 1.52 | 4.44 | 4.94 |
| 21:00 | 1477 | VVV Venlo vs ADO Den Haag | 2.61 | 3.55 | 2.38 |
| 21:00 | 2451 | Dordrecht vs FC Eindhoven | 4.64 | 3.80 | 1.65 |
| 21:00 | 2846 | Roda Kerkrade vs Jong Utrecht | 1.23 | 5.91 | 9.65 |
| 21:00 | 3884 | Helmond Sport vs Maastricht | 1.97 | 3.70 | 3.25 |
| 21:00 | 4642 | Jong AZ Alkmaar vs Jong PSV | 2.81 | 3.50 | 2.26 |
| 21:00 | 4777 | Almere City vs SBV Excelsior | 2.41 | 3.56 | 2.57 |
| 21:00 | 4938 | Telstar vs Den Bosch | 1.79 | 3.75 | 3.85 |
| 21:00 | 5466 | De Graafschap vs Emmen | 2.71 | 3.15 | 2.51 |
| 21:15 | 5512 | FC Wil vs FC Aarau | 3.20 | 3.74 | 1.92 |
| 21:25 | 1654 | Liebherr Gak vs Blau Weiss Linz | 3.26 | 3.36 | 2.02 |
| 21:30 | 2205 | Slask Wroclaw vs Lech Poznan | 5.23 | 3.58 | 1.59 |
| 21:30 | 3653 | Union Berlin vs FC Koln | 2.37 | 3.25 | 2.95 |
| 21:30 | 4582 | Podbeskidzie Bie vs LKS Lodz Pss | 2.23 | 3.30 | 2.86 |
| 21:45 | 1100 | Kfco Wilrijk vs Brugge | 8.97 | 5.58 | 1.28 |
| 21:45 | 1278 | Hull City vs Huddersfield | 2.73 | 3.13 | 2.53 |
| 21:45 | 1539 | Ayr United vs Hamilton | 2.30 | 3.20 | 2.95 |
| 21:45 | 1700 | Edinburgh City vs Kelty Hearts FC | 5.06 | 3.90 | 1.55 |
| 21:45 | 1856 | Dundalk FC vs UCD Dublin | 1.33 | 4.58 | 7.59 |
| 21:45 | 2102 | Wexford Youths vs Cork City | 3.70 | 3.50 | 1.84 |
| 21:45 | 2578 | Bohemians FC vs Derry City | 2.73 | 3.02 | 2.48 |
| 21:45 | 3094 | Waterford Utd vs Longford Town | 1.56 | 3.83 | 5.04 |
| 21:45 | 3124 | Morton vs Kilmarnock | 3.40 | 3.20 | 2.09 |
| 21:45 | 3131 | St Patricks vs Drogheda Utd | 1.35 | 4.38 | 7.59 |
| 21:45 | 4236 | Cliftonville Belfast vs Crusaders Belfast | 2.20 | 3.45 | 2.82 |
| 21:45 | 4320 | Athlone Town vs Bray Wanderers | 3.99 | 3.65 | 1.74 |
| 21:45 | 5815 | Galway United vs Cobh Ramblers | 1.50 | 3.99 | 5.46 |
| 21:45 | 5967 | Sligo Rovers vs Shelbourne | 1.73 | 3.36 | 4.48 |
| 22:00 | 1347 | Finn Harps vs Shamrock Rovers | 5.25 | 3.45 | 1.61 |
| 22:00 | 1607 | Girona vs Malaga | 1.60 | 3.67 | 5.55 |
| 22:00 | 5434 | Metropolitanos vs Carabobo FC | 1.94 | 3.30 | 3.95 |


# ADEBAYOR TUTALAMBA DUME - SIMBA

**Na Adam Fungamwango**



KLABU ya Simba imesema kuwa iwapo ikimpata kiungo mshambuliaji raia wa Niger, Victorien Adebayor, basi itakuwa imelamba dume kwa sababu ni mchezaji mwenye uzoefu mkubwa kwenye michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally amesema mchezaji huyo ni aina ya wachezaji ambao Klabu ya Simba inawataka kwani hawasubiri mpaka wazoee mazingira.

"Sijajua kwa viongozi wa juu wanafikiria nini, lakini nikiri kuwa Adebayor ni aina ya mchezaji ambaye kama tunampata anakwenda kuongeza kitu kwenye kikosi chetu, kwanza ana uzoefu wa kutosha, ana uwezo mkubwa na ni mchezaji bora kwenye mechi za kimataifa.

"Si aina ya mchezaji ambaye anakuja kwenye klabu anaanza kushangaashangaa kwanza mpaka asome mazingira, azoee, hapana, huyu tayari ana uzoefu wa kutosha, tukimpata Wanasimba tutakuwa tumelamba dume," alisema Ahmed.

Mchezaji huyo alitarajiwa kuwasili jana nchini kujiunga na kikosi cha timu yake ya US Gendarmarie ambacho kiliwasili tangu juzi nchini kwa ajili ya mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kati ya timu hizo mbili.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema kuwa atamwambia Rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji 'kuvunja benki' ili kumsajili mchezaji huyo kwa ajili ya msimu ujao wa ligi na mechi za kimataifa.

Naye, akizungumzia usajili hivi karibuni, Dewji alisema hivi sasa wameshakuwa na uzoefu na soka la Afrika, hasa kuhusu usajili, hivyo wanapofanya kazi hiyo kwa sasa huwa hawapigi kelele, wala kusemasema kwenye vyombo vya habari.

Tetesi zinaeleza kuwa Simba ilikuwa inamhitaji pia raia wa Burkina Faso, Stephano Aziz Ki anayechezea Asec Mimosas, lakini dili linaonekana kukwama kutokana na mchezaji huyo kupata timu mbili nje ya bara la Afrika ambazo zinamuwania.

# Geita, Mbeya City kazi ipo kesho

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la Klabu ya Geita Gold limesema wapo imara na tayari kuelekea kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya NBC dhidi ya Mbeya City utakaopigwa kesho, Jumamosi katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Filex Minziro, alisema mchezo huo unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa, lakini wamejipanga vema kukabiliana na wapinzani wao hao.

"Mchezo utakuwa mgumu nina uheshimu, tunapaswa kuingia kwa tahadhari ili kuweza kupata matokeo chanya," alisema Minziro.

Alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri na mazoezi kuelekea mechi hiyo ambayo kama wakishinda itawafanya kufikisha ponti 24 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Aidha, Minziro alisema mikakati yao ni kufanya vizuri kwenye kila mchezo ili msimu ujao waendelee kushiriki Ligi Kuu ya NBC.

Alisema mapumziko mafupi ya kupisha Kalenda ya Fifa, kwa upande wa wachezaji wake yamewasaidia kuzidi kujiweka sawa kwa ligi hiyo.


Geita Gold ipo nafasi ya tisa kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 21 wakati Mbeya City yenyewe ina pointi 25 katika nafasi ya tano baada ya timu zote kushuka dimbani mara 18 msimu huu.



Michezo

Ijumaa Aprili 1, 2022

Nipashe



## Dybala achagua kwenda kuitumikia Atletico Madrid

MSULI MSULI TU...



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. Timu hiyo itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili saa 4:00 usiku kuikaribisha US Gendarmerie ya Niger kwenye mechi ya mwisho ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: MAKTABA**

# CAF WAPINDUA MECHI SIMBA, GENDARMERIE

●●●Yazipeleka 'machinjioni' saa 4 usiku, Chama cha Usafirishaji cha ahidi usafiri kwa mashabiki, Jeshi la Polisi ulinzi mkali, huku...

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka Afrika (CAF), limefikia uamuzi wa muda wa mechi za mwisho za hatua ya makundi hususan ya Kundi D kati ya Simba na US Gendarmerie ya Niger na ile ya RS Berkane ya Morocco dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Tayari mechi zote za hatua ya makundi hususan makundi mengine matatu A, B na C, muda ulishapangwa isipokuwa Kundi D, uamuzi wa muda wa kuchezwa mechi hizo mbili ulikuwa haujafikiwa rasmi.

Ikumbukwe timu zote katika Kundi D, zina nafasi ya kufuzu robo fainali wakati huu Asec Mimosas ambayo itakuwa ugenini dhidi ya RS Berkane, ikiongoza kundi hilo kwa alama zake tisa huku Simba na Wamorocco hao kila moja ikiwa na alama saba na Gendarmerie ikiburuza mkiani kwa pointi tano.

Simba na RS Berkane zinahitaji ushindi ili kutinga robo fainali wakati Asec Mimosas wenyewe sare tu ikiwatosha kusonga mbele, huku Gendarmerie wakitakiwa kushinda na wakati huohuo wakiwaombea Wamorocco hao kupoteza.

Awali, mechi ya Simba na Gendarmerie ilipangwa kuchezwa saa 1:00 usiku ambapo kwa Morocco ni saa nane mchana, lakini kwa sababu michezo yote inatakiwa kuchezwa muda mmoja ili kuepuka upangaji wa matokeo, RS Berkane iliomba kufanyika mabadiliko ili wachezaji wake wawe wameshapata futari.

Hata hivyo, mjadala wa muda uliendelea na jana saa nane mchana CAF ikafanya maamuzi ya mechi ya Simba na Gendarmerie kupigwa saa 4:00 usiku ambapo kwa Morocco itakuwa saa 2:00 usiku, muda ambao tayari watakuwa wamepata futari.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia gazeti hili kuwa maandalizi kuelekea mchezo huo yamekamilika na wanawaahidi mashabiki ulinzi wa kiwango cha juu utakuwapo ndani na nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kuwa tayari wamehakikishiwa hilo kutoka Jeshi la Polisi nchini.

"Nawakaribisha Wanasimba wote kuja uwanjani muda huo kuishangilia timu yao, tumezungumza na Jeshi la Polisi wamesema wataongeza askari wengi hasa eneo la nje ya uwanja ili kuimarisha usalama," alisema Ahmed.

Aidha, Ahmed alisema pia Simba imekubaliana na Chama cha Wasafirishaji Dar es Salaam kuhakikisha wanatoa huduma ya usafiri kwa ajili ya kuwaleta na kuwarejesha nyumbani mashabiki kutoka kila kona ya Dar es Salaam.

Akizungumzia kauli hiyo ya Ahmed, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Madereva Tanzania (TADU), Jaeka Odillo Mdami, alisema: "Usafiri utakuwapo hadi saa sita usiku, tutawapeleka maeneo yote wakazi wa Jiji la Dar es Salaam ambao watakuwapo uwanjani siku hiyo. Usafiri wa Kibaha pia utakuwepo."

## Aucho, Fei Toto kuikosa Azam

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema kuwa wachezaji Khalid Aucho na Feisal Salum "Fei Toto', wataukosa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu hiyo na Azam FC utakaopigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam kutokana na kuwa majeruhi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Kaze raia wa Burundi, alisema kuwa 'Fei Toto" amepewa siku 10 za matibabu na mapumziko baada ya kugundulika kuwa ameumia, huku Aucho akiumia akiwa na kikosi cha timu ya Taifa ya Uganda.

"Aucho ana majeraha, ameyapata akiwa kwenye kikosi cha timu ya taifa, Uganda Cranes kwa hiyo akija inabidi kwanza afanyiwe vipimo ili tujue ukubwa wa maumivu au jeraha lake. Kwenye kikosi cha timu ya taifa hawakumfanyia vipimo na hilo hatujafurahishwa nalo, kwa sababu ilibidi wampime aje na ripoti ili awape madaktari wetu, kazi yao ingekuwa ndogo tu ya kuanza kumtibia, lakini siyo hivyo inabidi kwanza afanyiwe vipimo ijulikane ni kitu gani kinamsumbua," alisema kocha huyo.

Kuhusu Fei Toto alisema wamempa mapumziko ya siku 10, huku pia akipatiwa matibabu na baada ya hapo wataona nini kinaendelea.

"Hatutoharakisha kumtumia Fei Toto, ndiyo maana nasema anaukosa mchezo wetu dhidi ya Azam Aprili 6 kule Chamazi," alisema kocha huyo.

Kuhusu mechi yao dhidi ya Mafunzo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, kocha huyo alisema amejifunza vitu vingi, kwani ilikuwa ni mechi ya kuwapa nafasi wachezaji wengine ambao hawapati muda mrefu wa kucheza, pamoja na wale waliotoka kuuguza majeraha.

"Nimeifurahia mechi hii, tumepata picha ya kule tunakokwenda na nini kifanyike, kwani inawezekana ikawa ndiyo mechi yetu ya mwisho ya kirafiki msimu huu kutokana na mlundikano wa ratiba. Ilikuwa ni mechi ya kuwafanya wachezaji wacheze na kujiamini," alisema. Yanga ilishinda mabao 3-2 .

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >